JACKPOT BABA LAO!
TZS. 360,499,520
KWA TZS. 1000 TU!
SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!
SportPesa.CO.TZ
PIGA *150*87#



UKURASA 4

**ATINGA** Ikulu kudai kiwanja kilichouzwa miaka 25




UKURASA 9

Nipashe Jumapili
MWANGA WA JAMII
Jumapili Oktoba 2, 2022 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-
www.ippmedia.com
ISSN 0856 • No. 0581086
www.twitter.com/nipashetz
www.facebook.com/nipashetz
www.instagram.com/theguardian_newspaper
LIKE & FOLLOW US

# Daktari Mtanzania afa ebola Uganda

**MAABARA** tembezi yapelekwa Kagera..

*Endelea ukurasa 2*



Dk. Mohammed Ali

Waziri wa Afya Ummy Mwalimu

# Watumishi TANESCO mbaroni tuhuma utapeli Luku milioni 10/-

UKURASA 8





Fundi wa TANESCO, akikagua mita ya umeme kwa mteja ili kuwabaini waliojiunganishia huduma kinyemela kwa kutumia mafundi vishoka kupitia huduma bila malipo katika Kata ya Isagehe wilayani Kahama mkoani Shinyanga jana. Kulia ni moja ya mita mbovu zilizoibwa katika shirika hilo na kukutwa zimefungwa katika Kanisa la Kalval Assembel of God (ACG), huku nyaya zinazoruhusu mita kusoma zikiwa hazijaunganishwa na kuruhusu umeme kuingia moja kwa moja kwa mteja. **PICHA: SHABAN NJIA**

UKURASA WA 8

## UN YATOA TUZO 2 KWA RAIS SAMIA

RAIS Samia Suluhu Hassan ametangazwa mshindi wa tuzo mbili za Rais, ya Dhahabu ya Malengo ya Maendeleo Endelevu (SDG) na Amani ya Dunia...

## CHADEMA yataka viti maalum vya wazee bungeni

UKURASA 2

**MICHEZO** AZAM YALIA NA WAAMUZI IKIKUBALI KICHAPO MBEYA UK. 23

**MAONI, KATUNI** UK.6

# Ebola yaua daktari Mtanzania Uganda

**Na Waandishi Wetu**

SIKU tatu baada ya serikali kutangaza tahadhari ya ugonjwa wa ebola nchini, daktari bingwa wa kitanzania aliyekuwa Uganda, amefariki dunia, Wizara ya Afya imethibitisha.

Ni tukio linalochukua sura huku kukiwapo hatua za kiserikali za tahadhari, kuletwa maabara tembezi, operesheni ya elimu kwa umma na angalizo maalum kwa mikoa iliyo jirani na kulikoathirika.

Taarifa ya wizara hiyo iliyotolewa jana jioni, ikitiwa saini na Waziri wa Afya, Ummy Mwalimu na Waziri mwenzake wa Afya wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, Nassor Mazurui, ilitamka:

"Tarehe moja (jana) Wizara ya Afya, imepokea taarifa kutoka Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki ikitoa taarifa ya kifo cha Dk. Mohamed Ali Hafidh aliyekuwa akisomea udaktari bingwa wa upasuaji Uganda akitokea Tanzania."

Kwa mujibu wa taarifa hiyo, tangu mwezi uliopita katika wilaya nne za Uganda, zimeshapata wagonjwa 54 wa maradhi hayo na kati yao, 25 walifariki dunia.

"Tarehe 28 mwaka huu, tulitoa tamko la kuupa habari umma pamoja na kutoa tahadhari kuhusu ugonjwa huu kwa wananchi ikiwamo hatua za kuchukua ili kujikinga," ilisema.

Juzi jioni kwenye mjadala wa redio moja ya nje, Katibu Mkuu wa Wizara ya Afya, Prof. Abel Makubi alitaja hatua zinginezo ni serikali inaendelea na kampeni za kuelimisha umma ngazi ya chini kuhusu ugonjwa huo katika mikoa iliyoko hatarini zaidi, ukiwamo wa Kagera.

Vilevile, jana serikali ilitangaza kuweka maabara tembezi ya kupima virusi vya ebola katika Kituo cha Afya Kabyaire wilayani Misenyi, Kagera ambako ni mpakani na Uganda.

Mganga Mkuu wa Mkoa wa Kagera, Dk. Issessanda Kaniki, alisema mjini Bukoba kwamba serikali imeweka maabara hiyo tembezi kusaidia kupima virusi vya ebola, akitaja kwenye Kituo cha Afya Kabyaire.

Katika kikao na wadau wa afya cha kujadili mlipuko wa ebola, alisema kuna hospitali 12 zitakazotoa huduma ya matibabu ya ebola, yakiwa yametengwa maeneo maalum kwa ajili ya kutoa huduma wagonjwa hao katika vituo vyote vya afya mkoani humo.

"Mashine iliyofungwa kituo cha Kabyaire, baada ya mtu kupimwa virusi vya ebola, majibu yanatoka ndani ya saa mbili na wameletwa wataalamu wa afya wanne katika kituo hicho," alifafanua.

Dk. Kaniki alisema baada ya mtu kupimwa na kuonekana na dalili, kutakuwa na gari la wagonjwa kwa ajili ya kuwasafirisha kwenye vituo maalum.

Alisema kila halmashauri imetenga eneo la karantini kwa ajili ya kuwaweka washukiwa wa ebola na watoa huduma.

***Imeandaliwa na Romana Mallya (DAR) na Mary Geofrey (Kagera).**



Rais Samia Suluhu Hassan, akimuapisha Abubakar Amin Mrisha kuwa Jaji wa Mahakama Kuu, Ikulu Chamwino, mkoani Dodoma jana. **PICHA: IKULU**

# CHADEMA yataka viti maalum wazee bungeni

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

CHAMA cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) kimesema kuna haja kuwa na mwakilishi wa wazee bungeni ili kundi hilo lipate mtetezi katika chombo hicho cha kutunga sheria.

Mwenyekiti wa Baraza la Wazee wa chama hicho (BAZECHA), Hashim Juma Issa, alitoa rai hiyo jana wakati wa Kongamano la Baraza hilo lililofanyika jijini hapa.

Alisema kuwa ili kupata haki zao za msingi wanapendekeza wazee kuwa na mbunge mwakilishi wa kundi hilo.

Issa alisema hivi sasa imekuwa shida kero zao kusikilizwa bungeni, hivyo wanaona ipo haja kuwa na mbunge mwakilishi mahususi wa wazee katika chombo hicho chenye jukumu la kuishauri na kuikosoa serikali.

"Tunaomba tupate mwakilishi ambaye atatusemea mambo yetu kwani wazee tunakabiliwa na kero mbalimbali ikiwamo matibabu kutokana na umri wetu kukumbwa magonjwa ya mara kwa mara, pia tunataka uhakika wa matibabu bure isiwe siasa," alisema.

**JENERALI ULIMWENGU**

Katika kongamano hilo, mwandishi wa habari mkongwe, Jenerali Ulimwengu, aliyekuwa amealikwa kushiriki, aliishauri serikali kupunguza matumizi yake ikiwamo ununuzi wa magari ya kifahari (V8), posho na misafari mirefu ya viongozi wa umma isiyokuwa na tija ili kuwa na fedha zitakazotumika kutatua kero za wananchi likiwamo kundi la wazee.

Ulimwengu alisema ipo haja kwa serikali kupunguza matumizi katika maeneo mengi ili kuwa na fedha ambazo zitatumika kuhudumia wananchi wakiwamo wazee ambao wametumia muda wao mwingi kulitumikia taifa.

"Wazee wetu hawa walimetumikia taifa kwa uzalendo mkubwa kweli, wapo baadhi yao ambao hawakutimiza wajibu wao lakini kwa umuhimu wao, serikali inatakiwa kuweka mkakati wa kuwahudumia ikiwamo kuwalipa pensheni ya kila mwezi wazee wote nchini," alisema Ulimwengu.

Alisema serikali itaweza kufanya hivyo kama itapunguza matumizi katika ununuzi wa magari ya kifahari, malipo ya posho na misafara mirefu ya viongozi wa umma ambayo alidai haina tija kwa taifa.

Alisema kama serikali ikiamua kupunguza matumizi hayo, fedha za pensheni ya kuwalipa wazee itapatikana.

Aliwataka Watanzania kujenga jamii ya haki na usawa kwa kuhakikisha maslahi ya wazee yanalindwa kwa kuondoa unyanyapaa, chuki na dharau.

Ulimwengu pia aliwataka vijana kujifunza kwa wazee kwa kuwa wanayo maarifa mengi yatakayowasaidia katika maisha yao na taifa kwa ujumla.

"Vijana badala ya kwenda baa kunywa pombe, mkikaa na wazee mtajifunza mambo mengi sana kwani ninaamini mzee mmoja akifa, basi ni sawa na maktaba ndogo imeungua na moto kwani maarifa aliyonayo na uzoefu wa mambo mbalimbali anakufa nayo," alisema.

Ulimwengu alipongeza CHADEMA kwa kufanya mkutano huo wa Baraza la Wazee bila kuomba fedha kwa wadhamini wala wafanyabishara wakubwa kama ilivyo kwa vyama vingine vya siasa.

## India kuisadia Tanzania mkakati uchumi wa buluu

**Na Romana Mallya**

INDIA imesisitiza nia yake ya kuisaidia Tanzania kufikia malengo ya uchumi wa buluu kwa kuwasaidia Watanzania wanaotaka kusoma mambo ya bahari kupelekwa nchini humo kuyasomea.

Akizungumza jana wakati wa kongamano la siku mbili la kimataifa linalohusu ushirikiano baina ya Tanzania na India, Balozi wa India nchini, Binaya Pradhan, alisema wako tayari kushirikiana na Tanzania katika eneo hilo.

Alisema India inatambua dhamira ya dhati ya Rais Samia Suluhu Hassan ya kuhakikisha Tanzania inafikia uchumi wa buluu, hivyo wako tayari kusaidia kwa wale wanaotaka kusoma mambo yanayohusiana na bahari.

Balozi huyo alisema wamezungumza na Kaimu Mkuu wa Chuo cha Bahari Dar es Salaam (DMI), Dk. Tumaini Gurumo kuwa kila mwaka ubalozi huo umekuwa ukitoa ufadhili wa masomo kwa takriban Watanzania 700, lakini katika eneo la mafunzo ya bahari hawajitokezi.

"Tunapendekeza wanafunzi wenye nia ya kwenda kusoma India kujitokeza, tutaweka utaratibu wa kusoma kwenye vyuo bora na ufanisi wa hali ya juu vinavyotoa mafunzo ya bahari," alishauri.

Pia alisema katika mkutano huo wamezungumzia mambo mengine mbalimbali yakiwamo yanayohusu maeneo ya kimkakati, uchumi, utamaduni na kuangalia wanayoweza kuyaongeza katika ushirikiano huo.

Dk. Gurumo alisema: "Uhitaji ni mkubwa wa watu wenye weledi wa kufanya kazi katika sekta hii ya uchumi wa buluu. Chuo chetu kina uhitaji mkubwa wa walimu mabaharia na wengine waliobobea katika masuala ya bahari, lakini hawapatikani kwa sababu elimu hiyo imekuwa haitolewi nchini."

Alisema elimu hiyo hupatikana kwa wenye uwezo au kupitia ufadhili wa masomo yanayotolewa nje ya nchi kwa sababu gharama za masomo ni kubwa ambazo zinaanzia Sh. milioni 60 hadi milioni 150.

"Uhitaji huu nimeutaja kwa chuo chetu, lakini ukienda Shirika la Uwakala wa Meli Tanzania (TASAC) ambao ndiyo wasimamizi wa masuala ya bahari, hata wao wana uhaba wa watumishi waliojikita katika weledi wa masuala ya bahari kati maeneo mbalimbali," alisema.

Akizungumzia ushirikiano kati ya nchi hizo mbili, Mtendaji Mkuu wa Taasisi ya Sanaa na Utamaduni Bagamoyo, Dk. Herbert Makoye, ambaye alikuwa mgeni rasmi, alisema ipo mikataba mbalimbali iliyotiwa saini na inayoendelea kutiwa saini na kinachofanywa na serikali ni kuhakikisha inafikia malengo yaliyoainishwa ndani yake.

**HABARI KITAIFA**

# Mapato ya utalii yazidi kuongezeka

**Na Lusungu Helela**

MAPATO yatokanayo na utalii yameongezeka kutoka Dola za Kimarekani milioni 714.59 kwa mwaka 2020 hadi Dola za Kimarekani milioni 1,310.34 kwa mwaka 2021.

Taarifa iliyotolewa juzi jijini Arusha na Mwenyekiti wa Kamati ya Ripoti ya Utafiti wa Watalii ambaye ni Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Maliasili na Utalii, Juma Mkomi, wakati wa uzinduzi wa ripoti ya Matokeo ya Utafiti wa Watalii Walioondoka nchini mwaka 2021, ilibainisha hayo.

Mkomi alisema taarifa ya utafiti huo inaonesha kuwa Tanzania inazidi kufanya vizuri katika utalii huku mapato yatokanayo na sekta hiyo yakiongezeka mwaka hadi mwaka.

Alisema mwaka mmoja baada ya mlipuko wa janga la UVIKO-19, idadi ya watalii iliongezeka kutoka 620,867 mwaka 2020 hadi kufikia watalii 922,692 mwaka 2021, sawa na ongezeko la asilimia 48.6.

Mwenyekiti huyo alizitaja sababu zilizochangia ongezeko la watalii nchini baada ya mlipuko wa UVIKO 19 kuwa ni jitihada zinazofanywa na serikali pamoja na sekta binafsi katika kutangaza vivutio vya utalii ndani na nje ya nchi.

Mkomi alisema matokeo ya utafiti yanaonyesha idadi kubwa ya watalii walifika nchini kwa ajili ya kutembelea hifadhi za wanyamapori na fukwe.

Utafiti huo umefanywa na Wizara ya Maliasili na Utalii kwa kushirikiana na Benki Kuu Tanzania (BOT), Ofisi ya Taifa ya Takwimu (NBS), Idara ya Uhamiaji, Kamisheni ya Utalii Zanzibar na Shirikisho la Wawekezaji katika Sekta ya Utalii Zanzibar ( ZATI).

Alisema takwinu za utafiti huo, zimepatikana kutokana na utafiti uliofanywa katika vituo vikubwa vinane vya watalii, vikiwemo viwanja vya ndege vya kimataifa na maeneo ya njia za kuingilia na kutokea watalii.

"Matokeo ya utafiti huo yameonyesha kuwa idadi kubwa ya watalii wametokea nchi ya Ufaransa ikifuatiwa na Marekani, Kenya na Zambia," alibainisha.

Katika hatua nyingine, Mkomi alisema matokeo ya utafiti huo yameonyesha kuwa wastani wa matumizi ya mtalii kwa siku nchini yaliongezeka kutoka Dola za Kimarekani 152 mwaka 2020 hadi kufikia Dola za Kimarekani 199 mwaka 2021

Naye Kaimu Mkurugenzi wa Utalii katika Wizara ya Maliasili na Utalii, Richie Wandwi, amesema kwa sasa wizara imejizatiti kuwekeza nguvu katika utalii wa fukwe kwa vile ni aina ya utalii ambao unaonekana kupendwa na watalii wengi wanaoingia nchini.



Aliongeza kuwa Wizara itaendelea kuzifanyia kazi changamoto mbalimbali ambazo baadhi ya watalii wamekutana nazo ili kuhakikisha idadi ya watalii inazidi kuongezeka na vivutio vilivyopo nchini vinatangazwa kwa kasi zaidi katika jumuiya za kimataifa.

Utalii ni miongoni mwa sekta muhimu katika uchumi wa dunia ambapo idadi ya watalii duniani iliongezeka kwa takribani asilimia tano na kuchangia asilimia 6.8 ya mauzo ya nje na kuzalisha ajira milioni 333.

# LHRC yataka kiini cha mauaji ya wazee

**Na Augusta Njoji,**
DODOMA

RIPOTI ya utafiti wa Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC) imeonyesha Tanzania ni nchi ya pili Afrika kwa imani za kishirikina, hali inayochochea mauaji ya watu mbalimbali wakiwamo wazee.

Mkuu wa Kitengo cha Utafiti wa LHRC, Fundikila Wazambi, alibainisha hayo juzi alipowasilishaji mada kuhusu hali ya haki za binadamu nchini wakati wa mkutano wa wadau wa masuala ya wazee nchini uliofanyika jijini hapa.

Alisema ripoti hiyo ya mwaka 2017 ambayo ilikuwa inazungumzia masuala ya imani kwa Afrika, Cameroon ikiongoza ikifuatwa na Tanzania kwenye mambo ya imani za kishirikina.

"Hata kama hawaendi kwa waganga, wanaamini hiki kitu kikitokea nitakuwa nimerogwa. Kwa hiyo, wapo radhi kudanganywa na waganga kutokana na imani hiyo.

"Mtu akiugua, anakwenda kwanza kwa mganga kabla ya hospitalini, na haya ndiyo matokeo ya kutafutana uchawi na kusababisha mauaji kutokana na kupenda sana ramli,"alisema.

Wazambi alisema Tanzania inashika nafasi hiyo kutokana na ukubwa wa matukio yanayohusishwa na imani za kishirikina ambapo kwa kipindi cha Julai 2017 hadi Mei 2018 kulikuwa na mauaji ya wazee 117.

"Mauaji haya yalihusisha wanaume 91 na wanawake 26 na Mkoa wa Tabora uliongoza kwa kuwa na matukio mengi zaidi," alibainisha.

Wazambi alisema kwa kipindi cha mwaka 2021 kumekuwa na matukio 155 yaliyoripotiwa kuvunjwa kwa haki za wazee na matukio 16 yaliyoripotiwa wazee kuvunjiwa haki kingono pamoja na kunyang'anywa mali.

Alisema tatizo pia lipo kwa kundi la vijana ambalo halitaki kufanya kazi na badala yake linatafuta njia za mkato kupata mafanikio.

Akitoa taarifa ya utafiti wa hali ya wazee uliofanywa kwa nchi 12 duniani, Meneja Programu, Haki, Sera na Ushirikiano wa Wadau wa Shirika la HelpAge International nchini, Joseph Mbasha, alisema kutokuwapo kwa Sheria ya Wazee ni sehemu ya maficho ya ukatili na manyanyaso dhidi ya wazee.

Alisema Tanzania inayo Sera ya Wazee ya Mwaka 2003, lakini tangu wakati huo sheria haijatungwa.

"Takwimu za Sensa ya Watu na Makazi ya Mwaka 2012 zinaonyesha kuna wazee 2,507,568 Tanzania lakini hakuna utekelezaji wa haki za wazee hasa katika ulinzi, haki na ustawi wao," alisema.

Mbasha aliongeza: "Kila mtu ni mzee ajae, matokeo ya utafiti yanashauri ili tuweze kuondoa vikwazo dhidi ya wazee, tunatakiwa kuwa na sheria, sera na mifumo madhubuti kushughulikia haki za wazee".

Kuhusu mfumo na muundo wa haki za wazee kwa kuzingatia itifaki ya haki za kundi hilo, Mkurugenzi kutoka Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora (THBUB), Joshua Taramo, alisema wazee wengi wanalalamikia masuala ya umiliki wa ardhi na mafao.

"Kwa sasa Tanzania ina zaidi ya sera 13 za wazee, sheria kuu zilizopitiwa zaidi ya 21 ambazo zinataja masuala ya wazee.

Pia kuna sheria za nyongeza 21 ambazo ni mfumo mzuri wa sheria," alisema.

Aliongeza kuwa pamoja na Rais Samia Suluhu Hassan kuzungumza kuhusu masuala ya wazee, ni wakati mwafaka sasa kupata sheria kwa ajili ya kundi hilo.

Mjumbe wa Jukwaa la Wahariri (TEF), Neville Meena, alisema uzee umekuwa unapuuzwa na kudharauliwa kwa njia nyingi na unapigwa vita.

"Vyombo vya habari vina wajibu wa kulilia kutungwa sheria kwa kuwa sera imekuwapo kwa miaka 20 sasa, tuna wajibu wa kushawishi, tuonyeshe tatizo ili kuzibwa na kuwapo kwa sheria," alisema.



# CCM yaipongeza NMB kusaidia huduma afya

Na Mwandishi Wetu

CHAMA Cha Mapinduzi (CCM) kimempongeza Rais Samia Suluhu Hassan kwa kugusa maisha ya wananchi kupitia mpango wa bima ya afya kwa wote kwa kuwa utawasaidia wengi kupata huduma za matibabu kwa uhakika.

Vilevile, chama hicho kimeipongeza Benki ya NMB kwa kuendelea kushiriki masuala ya kijamii yakiwamo yanayohusu afya ambayo ni muhimu kwa wananchi.

Pongezi hizo zilitolewa jana na Katibu wa Halmashauri Kuu ya Taifa (NEC) ya CCM Itikadi na Uenezi, Shaka Hamdu Shaka baada ya kukaribishwa na Waziri Mkuu Kassim Majaliwa, kutoa salamu za chama katika mbio zilizoandaliwa na NMB kwa ajili ya kuchangia matibabu ya wagonjwa wa Fistula walioko katika Hospitali ya CCBRT jijini Dar es Salaam.

"Waziri Mkuu kwa kutambua matibabu haya yana gharama kubwa, Ilani ya Uchaguzi ya CCM Ibara ya 83(e) inaelekeza katika kipindi cha miaka mitano, tutahakikisha kwamba tunaweza mazingira rafiki ya upatikanaji wa huduma hizi za afya.

"Nichukue fursa hii kwa niaba ya CCM kumpongeza kwa dhati kabisa Rais Samia Suluhu Hassan na serikali anayoiongoza kwa kuweka mpango madhubuti ya bima ya afya kwa wananchi wote," Shaka alisema.

Aliongeza kuwa wakati NMB wakishiriki jitihada katika kuimarisha sekta ya afya kwa kukusanya Sh. milioni 600, Rais Samia ameshaweka miundombinu ya kuhakikisha kwamba wananchi wote wanapata huduma hizo kupitia bima ya afya ili kupunguza makali ya upatikanaji wa huduma hizi.

"Ndugu zangu ninataka niwahakikishie kuwa hamtajutia uamuzi wa kuiamini serikali ya CCM. Kwa niaba ya CCM niwaahidi kwamba chama kitaendelea kuziunga mkono taasisi zote zinazounga mkono juhudi za maendeleo. Kazi ni moja na kazi inaendelea bila ya kurudi nyuma," alisema.

Shaka alisema Ilani ya Uchaguzi ya CCM Ibara ya 83, imeelekeza kwamba ndani ya kipindi cha miaka mitano, serikali itaimarisha huduma za afya kwa wananchi, ikiwa sambamba na ujenzi wa vituo vya afya, upatikanaji wa vifaa tiba na kuimarisha miundombinu ya maeneo ya kutolea huduma za afya.

"NMB hongereni sana kwa kuunga mkono jitihada za utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi," Shaka aliipongeza benki hiyo kwa namna ambavyo imeweka mipango na utaratibu wa kuishirikisha jamii katika masuala mbalimbali ya kijamii, akifafanua:

"Kitendo cha kuandaa tukio hili kutafuta fedha kwa ajili ya changamoto inayowakabili baadhi ya kinamama nchini ni hatua kubwa na ya kupongeza sana.

"Fistula imekuwa ikiwakosesha kujiamini na imekuwa ikiwakosesha furaha baadhi ya kinamama, huu leo ni ukombozi wa kurudisha heshima, kurudisha utu na kurudisha kujiamini kwa baadhi ya kinamama ambao wanapambana na changamoto hii."

Ofisa Mtendaji Mkuu wa NMB, Ruth Zaipuna alisema mbio hizo zilianzishwa mwaka jana zikiwa na lengo la kukusanya Sh. bilioni moja katika kipindi cha miaka minne.

"Tulijiwekea lengo la kukusanya Sh. milioni 600 katika kipindi cha miaka miwili, na leo nina furaha kukutaarifu kuwa tumefikia lengo ndani ya miaka miwili. Tunakwenda kusaidia wanawake wengi walioko CCBRT ambao hawana uwezo wa kugharimia matibabu," alisema.

Spika wa Baraza la Wawakilishi, Zubeir Ali Maulid aliwashukuru waandaaji Benki ya NMB kwa kuona umuhimu wa kuishirikisha pande zote mbili za Muungano.



Asha Ibrahimu ambaye ni mlemavu wa miguu, mkazi wa kijiji cha Unyabwa, Manispaa ya Singida, akilia mbele ya Mkuu wa Mkoa Singida, Peter Serukamba, baada ya kukabidhiwa hati ya kiwanja alichosotea kwa miaka 25 kufuatilia ofisi mbalimbali za serikali hadi Rais Samia Suluhu Hassan alipoamuru apewe kiwanja haraka. **PICHA: THOBIAS MWANAKATWE**

# Atinga Ikulu kudai kiwanja chake kilichouzwa miaka 25

**Na Thobias Mwanakatwe,** SINGIDA

RAIS Samia Suluhu Hassan amemsaidia Asha Ibrahimu (53), mkazi wa Kijiji cha Unyabwa, Manispaa ya Singida kupata kiwanja chake ambacho amesota kukifuatilia kwa miaka 25 baada ya manispaa hiyo kukiuza kwa mtu mwingine.

Asha mwenye ulemavu wa miguu, wakati akikabidhiwa juzi na Mkuu wa Mkoa wa Singida, Peter Serukamba hati ya kiwanja kipya, aliangua kilio kwa furaha katika Ofisi ya Mkuu wa Mkoa mjini hapa.

Kiwanja alichokabidhiwa kiko eneo la Unyankindi, Manispaa ya Singida baada ya Rais kuuagiza uongozi wa Mkoa wa Singida apewe kiwanja kingine kutokana na kile cha awali alichokuwa akikimiliki kihalali na kulipia kodi ya ardhi miaka minne mfululizo, kuuzwa kwa muuguzi,

Alisema alibaini kiwanja chake namba 217 kitalu B kuuzwa mwaka 1997 alipokwenda kumwaga kokoto, mchanga na mawe kwa ajili ya kuanza ujenzi, akielezwa na maofisa ardhi kuwa kiwanja chake kimemilikishwa mtu mwingine na kumwahidi kumpatia kingine ndani ya muda mfupi.

Alisema alianza kufuatilia suala hilo kwa viongozi mbalimbali wa Manispaa ya Singida, Wilaya ya Singida na mkoa lakini alikuwa akipewa ahadi zisizotekelezeka tangu Juni 2019 hadi ilipofika Aprili 4, 2022 alipoamua kwenda Ikulu Chamwino mkoani Dodoma kwa lengo la kuonana na Rais.

Alisema kufika kwake Ikulu ingawa haikuwa rahisi na hakufanikiwa kuonana na Rais ana kwa ana, kumemsaidia kwa kuwa wasaidizi wa Rais walimsikiliza na hatimaye kutoa maagizo kwa viongozi wa Mkoa wa Singida kushughulikia suala hilo haraka.

Asha alisema katika miaka yote 25 ambayo amekuwa akifuatilia haki ya kiwanja chake, amekumbana na shida nyingi ikiwamo kupata ajali ya gari mwaka 2016 ambapo alivunjika nguu ambao sasa amekuwa na ulemavu na hawezi kutembea vizuri.

Aliongeza kuwa pamoja na kupewa kiwanja kingine ambacho akisotea kwa miaka 25, sasa hana uwezo wa kujenga kutokana na kupata ulemavu na kuwaomba wasamalia wema wamsaidie ili apate sehemu ya kuishi.

Pia alimshukru Rais Samia na viongozi wa Mkoa wa Singida kwa kumsaidia kupata kiwanja kipya.

Mkuu wa Mkoa wa Singida, Peter Serukamba, akizungumza wakati akimkabidhi hati ya kiwanja kipya, alisema alipata barua kutoka Ofisi ya Rais ikitoa maelekezo Asha apewe kiwanja kingine baada ya kile cha awali kuuzwa kwa mtu mwingine.

Alisema baada ya kupata barua hiyo, alikaa na viongozi wa Manispaa ya Singida ambao walikiri kiwanja cha Asha alichokuwa akikimiliki kihalali, kupewa mtu mwingine.

Serukamba alisema baada ya hapo aliwaagiza viongozi wa Manispaa ya Singida kumtafutia kiwanja kingine haraka Bi. Asha katika eneo atakalopenda, agizo ambalo limetekelezwa.

Mkuu huyo wa Mkoa alimwagiza Mkurugenzi wa Manispaa ya Singida kupeleka kokoto, mawe na mchanga katika kiwanja kipya alichopewa Asha kwa kuwa kile cha awali alichouziwa mtu mwingine kilikuwa na vitu hivyo.

# Wachangia mil. 56/-ujenzi wa mabweni

Na Joseph Mwendapole

CHUO cha Elimu ya Biashara (CBE) kimefanikiwa kukusanya Sh. milioni 56 kwa ajili ya ujenzi wa mabweni ya wasichana kwenye kampasi yake ya Mbeya, kikiwaomba wananchi kuendelea kuchangia ili kufanikisha ujenzi huo.

Ombi hilo lilitolewa jana jijini Dar es Salaam na Mkuu wa chuo hicho, Prof. Emmanuel Mjema, alipozungumza na waandishi wa habari na kutoa shukrani kwa wote waliochangia harambee hiyo iliyofanyika mwishoni mwa wiki iliyopita jijini Mbeya.

"Kwa niaba ya mlezi wa Kampasi ya CBE Mbeya, Dk. Tulia Ackson, Mbunge wa Mbeya Mjini na Spika wa Bunge, ninaomba niwashukuru wadau wote waliofika kwenye hafla za kilele cha harambee ya ujenzi wa mabweni ya wasichana Mbeya," alisema.

Pia alimshukuru na kumpongeza Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera aliyekuwa mgeni rasmi kwa kuendesha shughuli ya harambee hiyo na kuchangisha kiasi hicho cha fedha.

Alimshukuru Dk. Tulia ambaye pia ni mlezi wa Kampasi CBE Mbeya kwa kuanzishia na kusimamia harambee hiyo tangu alipoizindua yeye mwenyewe mwaka jana.

Alisema harambee hiyo inalenga kukusanya Sh. bilioni 1.2 kwa ajili ya ujenzi wa mabweni ya wasichana huku akitoa wito kwa wadau kuendelea kuchangia kwa kuwa wanahitaji fedha zaidi kufanikisha ujenzi huo.

"Kwa wale watakaoendelea kuguswa tutaendelea kupokea na kutambua michango yao kwa kutoa tuzo katika makusanyiko makubwa ya chuo chetu.

"Ninawashukuru pia wabunge ambao wameendelea kutoa michango yao ya hali na mali, ni vigumu kuwataja majina yao wote ila mwisho kabisa wa jambo hili tunaweza kutoa majina ya taasisi, kampuni na watu binafsi walioguswa na kampeni hii," alisema.

Aliwaomba wadau wote wenye mapenzi mema na maendeleo ya nchi waliopo ndani na nje kuendelea kuwashika mkono kwa kuchangia chochote ili kukamilisha harambee hiyo kwa kuendelea kumuunga mkono mlezi wa Kampasi ya CBE, Dk. Tulia.

"Niwaombe wadau wote ambao tumewafikia na ambao watapata ujumbe wetu kupitia vyombo mbalimbali vya habari kwamba kwa wale wanaoendelea kuguswa na jambo hili tutaendelea kupokea na kutambua michango yao wakati ujenzi wa hosteli unaendelea," alisema.

Katika hatua nyingine, Prof. Mjema alisema kuwa Oktoba 8 mwaka huu 2022 watakuwa na hafla ya ufunguzi rasmi wa majengo na Kampasi ya CBE Mbeya ambapo mgeni rasmi katika hafla hiyo anatarajiwa kuwa Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa.

Prof. Mjema alisema hayo kwa wachangiaji wakubwa watakaojitokeza na wale ambao tayari watakabidhiwa tuzo zao siku hiyo.

HABARI KITAIFA

## Anna Henga: Kuna mfumo kandamizi dhidi ya wanawake

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

MKURUGENZI Mtendaji wa Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC), Anna Henga, amesema bado kuna mfumo kandamizi dhidi ya wanawake unaosababisha kushindwa kutafuta haki.

Anna aliyasema hayo juzi mjini hapa wakati wa kufunga wiki ya kutoa msaada wa kisheria ikiwa ni sehemu ya maadhimisho ya miaka 27 ya kuanzishwa kwa kituo hicho.

Alisema kuwa tangu kuzinduliwa kwa huduma za msaada wa kisheria mkoani humo, wananchi 796 wamefikiwa, asilimia 61 wakiwa ni wanaume.

"Kuna mwamko mdogo wa wanawake katika kutafuta haki na hii inakinzana na ukweli kwamba shida nyingi zinazotokea katika jamii kama matunzo ya watoto, migogoro ya ndoa na mirathi inahusisha zaidi wanawake.

"Tangu kuanzishwa huduma hii ya msaada wa kisheria mkoani hapa, migogoro ya ardhi ni 384, migogoro ya matunzo ya watoto na ndoa 109, mirathi 57, ajira na kazi 46 na migogoro mingine 47 na kesi za jinai zilikuwa 39," alibainisha.

Anna pia alitaja sababu ya kuongezeka kwa vitendo vya ukatili wa kijinsia hususani ubakaji na ulawiti zikijumuisha migogoro inayohusu ndoa.

Alisema migogoro ya ardhi inachochewa zaidi na uuzaji holela wa maeneo, uvamizi, maeneo kutwaliwa na kutolipwa fidia au kulipwa fidia ndogo na mingine inatokana na watu wengi kutokuwa na utamaduni wa kufungua mirathi.

Katibu Mkuu Wizara ya Katiba na Sheria, Mary Makondo, aliagiza kuanzishwa kwa vilabu vya haki za binadamu mikoa yote kuanzia shule za awali, sekondari, vyuoni hadi kazini.

"Vyombo vya habari tushirikiane katika kuhakikisha haki hizi tunazijua ipasavyo ili pale ambapo zimevunjwa, taarifa zifike na watoto wetu wawe salama, hususani katika janga hili la masuala ya ubakaji na ulawiti kwa watoto walioko shule za msingi na wengine wanafanyiwa majumbani, wote kwa pamoja tushirikiane," aliagiza.

Katibu Tawala wa Mkoa wa Njombe, Judica Omari, alisema jamii inapaswa kuthamini ndoa ambazo zinasimamiwa na dini mbalimbali kwa sababu ni chimbuko la kwanza la kusimamia haki.

# Bosi Magereza amulika mpasuko wa uongozi

**Na Renatha Msungu** DODOMA

KAMISHNA Jenerali wa Magereza Mzee Ramadhan Nyamka, amewaagiza Wakuu wa Magereza na Maofisa waandamizi wa jeshi hilo nchini kuhakikisha hakuna mpasuko ndani ya magereza.

Vilevile, amesisitiza kuwachukulia hatua kali maofisa watakaokwenda kinyume cha sheria ili kuwa na utendaji wenye tija ndani ya jeshi hilo.

Kamishna Jenerali Nyamka aliagiza hayo juzi alipofungua mkutano mkuu wa Wakuu wa Magereza na maofisa waandamizi wa jeshi hilo uliofanyika jijini hapa kwa ajili ya kujadili na kutathmini utendaji wao.

Alisema kuwa moja ya maagizo aliyopewa na Rais Samia Suluhu Hassan ni kuhakikisha watendaji wa Jeshi la Magereza wanakuwa pamoja na katika utekelezaji wa majukumu ya jeshi hilo na hatoruhusu kundi makundi ndani ya jeshi.

"Kama mnakumbuka Machi 25 mwaka huu Rais alifika Makao Makuu kwa ajili ya uwekaji jiwe la msingi na uzinduzi wa miradi yetu. Alizungumzia suala la mpasuko ndani ya Jeshi la Magereza. Katika mazingira kama haya. siyo rahisi watu kufanya kazi kwa tija," alionya.

Kamishna Jenerali alifafanua zaidi kuwa suala la nidhamu kwake ni kipaumbele na kuwataka wale ambao waliteleza, warudi kundini ili kuendeleza kazi za jeshi hilo kwa pamoja kwa manufaa ya jeshi na taifa.

"Kila zama na kitabu chake na nabii wake na hakuna katika mafundisho yanayosema kuna nabii alikuja kutengua yale ambayo nabii aliyepita aliyafundisha, hususani yakiwa mazuri, hivyo yale yaliyofanywa na viongozi wote wa jeshi hili walipita, hatuna budi kuyaendeleza," aliagiza.

Kamishna Jenerali aliongeza: "Baada ya kutoka kuapishwa wakati ninazungumza na watumishi wa Makao Makuu niliwaambia kwamba ninataka tuwe wamoja, kundi moja na wana Magereza wachapa kazi, isipokuwa makundi ya michezo yakiwapo ndani ya jeshi hayana tatizo."

Alisema viongozi wanalo jukumu kubwa la kuhakikishA wanafanya kazi kwa umoja, mshikamano na ushirikiano pamoja na kuwa na upendo wa hali ya juu ili wote waimbe wimbo mmoja na kuwa na uelekeo mmoja kiutendaji.

Awali akimkaribisha Kamishna Jenerali wa Jeshi hilo, Naibu Kamishna Jeremia Katungu aliwataka maofisa hao kuzingatia yale ambayo yatajadiliwa katika mkutano huo na kutekeleza maagizo ambayo watapewa na jeshi.

Alisema mkutano huo ni sehemu ya kupeana majukumu ya kila mmoja na mikakati ya namna ya kufanya kazi ili jeshi hilo lisonge mbele katika kazi zao za kila siku.



Diwani wa Kata ya Saranga, Manispaa ya Ubungo, Dar es Salaam, Edward Laizer, akizungumza katika mkutano wa mrejesho wa ufuatiliaji wa bajeti ya kata hiyo uliofanywa na Kituo cha Taarifa na Maarifa cha kata hiyo, juzi. Wengine ni Mwenyekiti wa Serikali ya Mtaa wa Stopover, Alex Msuka (kulia), Mwenyekiti wa Serikali ya Mtaa wa Upendo, Gwerino Kalinga (wa pili kushoto) na Mwenyekiti wa Kituo cha Taarifa na Maarifa cha kata hiyo, Maria Mwigune. **PICHA: SABATO KASIKA**

# ACT yataka Kikosi Kazi kizingatie maslahi umma

**Na Mwandishi Wetu,** MTWARA

KATIBU Mkuu wa ACT Wazalendo, Ado Shaibu amekitaka Kikosi Kazi cha Kuratibu Maoni ya Wadau Kuhusu Demokrasia kuzingatia maslahi mapana ya taifa na maoni ya wadau yaliyowasilishwa. Alitoa angalizo hilo jana alipozungumza na wanachama wa chama hicho katika Kijiji cha Kitama, Jimbo la Tandahimba mkoani Mtwara.

"Sisi ACT Wazalendo tuliamua tangu awali kutoa ushirikiano kwa Mheshimiwa Rais Samia (Suluhu Hassan) kwenye ajenda ya mageuzi ya kisiasa nchini. Tumeshawasilisha maoni yetu kwa Kikosi Kazi kuhusu Katiba Mpya, Tume Huru, Mageuzi ya Jeshi la Polisi na Tasnia ya Siasa kwa ujumla.

"Kikosi kazi kinapaswa kukamilisha kazi yake ili mageuzi ya msingi yaanze. Ni matumaini yetu kuwa Kikosi Kazi kwenye ripoti yake kitazingatia maslahi mapana ya umma, hasa katika kuhakikisha uchaguzi ujao unakuwa huru, wa haki na kuaminika na tasnia ya siasa inaendeshwa kwa usawa," alisema.

Katika hatua nyingine, Ado ameitaka Wizara ya Kilimo kuchukua hatua kushughulikia kero zinazolikabili zao la korosho nchini.

"Kwa miaka mingi sasa, korosho imekuwa. Zao kinara katika kuliingizia taifa fedha za kigeni ni kama limepuuzwa. Ni lazima serikali ishughulikie kero zinazolikabili zao hili ili wananchi wapate tija," alishauri Ado na kuongeza:

"Nimekuta wakulima wana kilio kikubwa cha pembejeo. Licha ya ahadi ya serikali kugawa pembejeo bure, kuna kilio kikubwa kuwa usambazaji haukuwa mzuri.

"Mfumo wa stakabadhi ghalani unalalamikiwa pia kwa kuchelewesha malipo na bei duni. Ni lazima Wizara ya Kilimo iyafanyie kazi masuala haya."

Kwa mujibu wa Janeth Joel Rithe, Naibu Katibu wa Habari, Uenezi na Mahusiano na Umma wa ACT Wazalendo, Ado alihitimisha ziara yake ya kata kwa kata katika Jimbo la Tandahimba na leo anatarajiwa kuanza ziara ya siku mbili ya ujenzi wa chama kwenye Jimbo la Tunduru Kusini.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Suala la lishe liwe shirikishi kuokoa vijana, kizazi kijacho

**KATIKA** vyombo mbalimbali vya habari jana, kulikuwa na habari inayomhusu Rais Samia Suluhu Hassan kuhusu mtindo wa maisha ya baadhi ya Watanzania hususan vijana. Mtindo huo ni matumizi ya dawa za kuongeza nguvu za kiume kutokana na aina ya vyakula wanavyokula vijana hao.

Rais Samia alitoa kauli hiyo juzi wakati wa kutia saini mkataba wa lishe jijini Dodoma huku akiweka bayana kwamba mtindo wa maisha hasa ulaji vyakula umewaharibu vijana wengi wa kiume na wa kike.

Bila kuuma maneno, mkuu huyo wa nchi alisema vyakula kama chipsi mayai vimewaathiri sana vijana jambo ambalo ni hatari kwa maendeleo ya taifa kwa kuwa kuna uwezekano mkubwa wa kuwa na kizazi goigoi siku zijazo.

Kutokana na vijana wengi kukosa nguvu za kiume, alisema baadhi yao wamejiingiza katika mkumbo wa kutumia dawa za kuongeza nguvu, maarufu kama 'vumbi la Congo' ambazo pia zina madhara makubwa kwa afya.

Sambamba na kutumia dawa hizo, vijana pia wamekuwa wakitumia vitu mbalimbali kama nazi, karanga na kubwa zaidi supu ya pweza kwa madai kwamba vitu hivyo vinaongeza nguvu za kiume.

Baada ya kubaini kuwa tatizo hilo ni kubwa, Rais Samia aliagiza wataalam kufanya utafiti kuhusu ukubwa wake na kutoa ushauri kwa kuwa kama tatizo hilo litaendelea, linaweza kuwa kubwa zaidi na matokeo yake taifa litakosa uzazi kwa kiwango kikubwa na hatimaye kuwa na vijana goigoi.

Kama alivyosema Rais Samia, mtindo wa maisha umeathiri vijana wengi wakiwamo walioko kwenye ndoa kushindwa kupata watoto kutokana na baadhi yao kukosa nguvu za kiume kulikosababishwa na ulaji vyakula ambavyo vinapunguza uwezo wa mwili kufanya kazi.

Migogoro ya ndoa hivi sasa limekuwa tatizo sugu kutokana na ukosefu wa nguvu za kiume kuwa moja ya sababu. Katika kudhihirisha hilo, kumekuwa na wimbi la talaka miongoni mwa wanandoa na hata mauaji baina yao yamekuwa yakiongezeka kwa sababu ya kukosekana kwa uaminifu.

Kwa kiasi kikubwa, mambo hayo yanasababishwa na baadhi ya wanandoa kuchepuka kwa sababu ya kutokutoshelewa na chanzo kikuu ni baadhi ya wanandoa wa kiume kukosa nguvu.


Pamoja na Rais kuagiza kufanyika utafiti, ni vyema elimu kuhusu lishe kwa ajili ya kujenga mwili imara kutolewa katika ngazi zote. Mkataba uliotiwa saini juzi kwa mikoa yote ni mwafaka lakini wadau pia watumie nafasi zao katika kuelimisha jamii, hasa vijana, juu ya ulaji wa vyakula vinavyostahili kujenga mwili.

Kwa kiasi kikubwa, elimu hiyo ilenge katika kubainisha ni vyakula gani vinapaswa kuliwa kwa kila rika kwa kuwa kuwapo kwa tabia ya ulaji vyakula kama chipsi mayai ambavyo ndivyo vinachangamkiwa kwa wingi na vijana, kunaendelea kuangamiza vijana na matokeo yake kutokuwapo kwa vizazi endelevu.

Viongozi wa dini kwa mfano, wanapaswa kutenga muda kwa ajili ya kutoa elimu maalum kwa vijana. Tunatambua kwamba baadhi ya madhehebu ya dini katika ibada yana vipindi kuhusu chakula na lishe, hivyo mengine yanatakiwa kuiga mfano huo ili kuokoa kizazi cha sasa kilichoko katika hatari ya kupotea na kuwa na akiba ya vizazi vijavyo.

Elimu itakayotolewa pia ilenge kuelezea madhara ya ulaji wa vyakula vinavyoweza kusababisha upungufu wa nguvu mwilini kwa vijana ambavyo huchochea kupungua kwa homoni muhimu kwa uzazi. Kwakuwa suala hili ni mtambuka, ni vyema kila mdau kwa nafasi yake akachukua jukumu kwa ajili ya maslahi ya taifa.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






Na Sabato Kasika

## Muungwana Lazima Nilonge

# Maeneo ya vijijini yapewe kipaumbele huduma hii ya afya

**HAPA** nchini, umeanzishwa mfumo wa usafirishaji wa dharura wa wajawazito na watoto wachanga uitwao M-MAMA, ambao unalenga kuwawahisha katika hospitali kwa ajili ya kupata huduma ya afya haraka iwezekanavyo.

Uwapo wa M-MAMA, ni miongoni mwa jitihada zinazofanywa na serikali, ili kunusuru wajawazito na watoto, lakini pia kwenye baadhi ya maeneo hasa vijijini ambako bado kuna changamoto ya mawasiliano.

Katika maeneo hayo ni kwamba hakuna mawasiliano ya haraka na usafiri wa uhakika wa kusaidia kumwahisha mama mjamzito kufika katika kituo cha afya, hali ambayo inaweza kufanya maisha yake kuwa rehani.

Hiyo inaonyesha kuwa kuna haja ya kuboresha barabara za vijijini ili ziweze kupitika wakati wote, ili inapotokea dharura, mjamzito aweze kuwahishwa katika kituo cha afya, apate huduma kwa wakati.

Wizara ya Afya inaeleza kuwa Tanzania itapokea msaada wa Dola za Kimarekani milioni 15, sawa na tariban Sh. bilioni 34 za Tanzania kutoka kampuni ya Vodafone, ili kuwezesha usafiri wa dharura kwa wajawazito.

Hiyo ni ahadi iliyotolewa hivi karibuni, katika kikao cha pembezoni cha Mkutano Mkuu wa 77 wa Wakuu wa Nchi (UNGA) New York, Marekani, ambapo Waziri wa Afya, Ummy Mwalimu, naye alihudhuria.

Kwa mujibu wa Ummy, Mkuu wa Masuala ya Kimataifa wa kampuni ya Vodafone, Joachim Reiter, aliwasilisha ahadi ya kampuni hiyo ya kutoa fedha hizo ili kutekeleza mradi huo ikiwa ni hatua ya kuunga mkono jitihada za Rais Samia Suluhu Hassan za kukuza uchumi wa nchi.

Ninadhani kwamba kuna haja kwa wizara kuelekeza fedha hizo maeneo ya vijijini kwa kupeleka magari ya wagonjwa huko, lakini pia kuboresha miundombinu ya barabara ili zipitike kirahisi wakati wote.

Serikali inabainisha kuwa takriban wanawake 4,000 na watoto 65,000 hufariki dunia kila mwaka huku kuchelewa kupata huduma za dharura ikiwa ni pamoja na usafiri wa dharura kukichangia sehemu ya vifo hivyo.

Kwa hiyo ninaamini kwamba iwapo fedha hizo zitapatikana, zinaweza kuwa msaada mkubwa wa kupunguza idadi hiyo ya vifo, hasa kwa kuboresha barabara na kuwapo magari ya kutosha ya kusafirisha wajawazito.

Waziri Ummy anabainisha kuwa mradi huo utaisaidia Tanzania kufikia malengo iliyojiwekea katika Mkakati wa Tano wa Afya na Mpango Mkakati wa Tatu wa Afya ya Uzazi, Mama na Mtoto (one plan 3) ambayo moja ya vipaumbele ni kupunguza vifo vya wajawazito na watoto.

Kwa maana hiyo, upatikanaji wa fedha hizo angalau ungekuwa chachu ya kuiwezesha nchi kuwa na barabara nzuri za kutosha maeneo ya vijijini, kwani hatua hiyo inaweza kusaidia kufikia malengo endelevu ya kidunia.

Kimsingi, karne hii ya 21, wajawazito kujifungulia nyumbani kutokana na ukosefu wa usafiri, ubovu wa barabara au kituo cha afya, si vyema, hivyo juhudi zinazofanywa na serikali zingesaidia upatikanaji wa huduma hizo.

Ninatambua juhudi za serikali za kuboresha huduma za afya ikiwa ni pamoja na kujenga zahanati kila kijiji, kituo cha afya kila kata na pia kujenga hospitali kila wilaya, lengo likiwa ni kusogeza huduma za afya karibu na wananchi.

Hatua hiyo inaweza kupunguzia wananchi kutembea umbali mrefu kufuata huduma ya afya, lakini pamoja na hayo, ni vyema kukawa na watumishi wa kutoka katika zahanati, vituo vya afya na hata hospitali za wilaya.

Kwa nini? Kwa sababu kumekuwapo na malalamiko kwenye baadhi ya zahanati na vituo vya afya, hasa maeneo ya vijijini, kwamba watumishi ni wachache kitendo kinachoweza husababisha huduma kuwa duni.

Hivyo, wakati serikali ikifanya kila inavyoweza kuhakikisha inapunguza vifo vya wajawazito na watoto, ingelitazama pia hilo suala la kuwapo kwa watumishi wa kutosha kwenye kada ya afya.

SAFU

FIKRA MBADALA

# Wabunge wapya Tanzania EALA waonyeshe uwezo kujenga hoja



Pascal Mayalla

Kwa Maslahi ya Taifa, inaendelea na makala elimishi za kuijua Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) na leo tunamalizia mfululizo huu kwa Sura ya Tisa. Sura hii inajumuisha Ibara ya 48 mpaka ya 65. Bunge la Afrika Mashariki ni chombo kilichaonzishwa ili kutekeleza majukumu ya kutunga sheria za Jumuiya.

Ibara ya 48 inahusu Muundo wa Bunge ambalo lina wajumbe tisa wa kuchaguliwa kutoka kila nchi na wajumbe tisa ambao wataingia kwa nyadhifu zao. Hawa ni mawaziri saba wa mambo ya nje kutoka katika nchi wanachama pamoja na Katibu Mkuu wa Jumuiya. Spika wa Bunge la Afrika Masharikí (EALA) atakuwa na madaraka ya kumwalika mtu yeyote ambaye mchango wake utahitajika katika kujadili hoja yoyote iliyowasilishwa mbele ya Bunge.

Ibara ya 53 inahusu Spika wa Bunge ikibainisha kwamba Spika atachaguliwa kutokana na wajumbe wa Bunge. Cheo hiki kitashikwa kwa mzunguko kati ya nchi wanachama.

Aidha, Ibara ya 49 inahusu Kazi za Bunge ambazo mbali na wajibu wa kutunga sheria, Bunge la Jumuiya litakuwa pia chombo cha kuendeleza uhusiano na mabunge ya kitaifa ya nchi wanachama kwa mambo yanayohusu jumuiya.

Bunge pia litakuwa na kazi ya kupitisha bajeti ya jumuiya. Kabla ya kupitisha bajeti, bunge litaangalia na kutathmini ripoti za shughuli za jumuiya. Kazi nyingine ya Bunge itakuwa kujadili mambo yote yanayohusu jumuiya na kupeleka mapendekezo kwenye Baraza la Mawaziri. Bunge litakuwa pia na kazi ya kupendekeza majina ya watu kwa ajili ya uteuzi wa nafasi za katibu mkuu na maofisa wengine wateule wa jumuiya.

**UTARATIBU WA KUTUNGA SHERIA**

Utungwaji wa sheria utaanza kwa kupelekwa muswada bungeni. Ikiwa muswada utapitishwa na bunge, Spika ataupeleka kwenye Mkutano wa Wakuu wa Nchi ili wautolee kibali. Wakuu wa nchi wakiukubali, unakuwa sheria na wakiukataa utahesabika kuwa umepitwa na wakati.

Kupitishwa kwa muswada wa sheria na wakuu wa nchi unataka makubaliano ya wakuu wote. Iwapo mkuu mmoja wa nchi atakataa, bado muswada huo hauwezi kupita.

**KANUNI ZA BUNGE**

Bunge lina uwezo wa kutengeneza kanuni zake, sheria na kanuni hizi zanaweza kuhusiana na uwezo, haki, kinga ya wabunge na utaratibu wa uendeshaji wa shughuli zake.

Miswada ya kupelekwa bungeni inaweza kupendekezwa na mjumbe yeyote. Lakini miswada hii iwe inahusiana na shughuli za Jumuiya na sheria zilizoainishwa katika Mkataba wa Jumuiya. Kwa upande wa Tanzania, tangu kuundwa kwa EALA, hakuna mbunge yeyote kutoka Tanzania, amewahi kupeleka muswada wowote!, Wabunge wa Kenya na Uganda pekee ndio wanaotamba.

**UCHAGUZI WA WABUNGE**

Wabunge wa Bunge la Jumuiya ya Afrika Mashariki watachaguliwa na Bunge la Taifa la kila nchi mwanachama. Kwa hiyo, kila anayetaka kugombea itabidi akapigiwe kura na Bunge la nchi yake. Kwa Tanzania si kila anayetaka, bali kila aliyepitishwa na chama cha siasa.

Kila nchi itachagua wabunge tisa, ambao watakuwa si wabunge katika bunge la nchi husika. Uteuzi wa wabunge hao utaangalia uwiano wa uwakilishi wa vyama mbalimbali vya siasa vilivyoingia katika bunge la nchi husika. Uteuzi utaangalia pia jinsia na uwakilishi mwingine muhimu katika kila bunge la nchi husika.

Sifa za kuchaguliwa kuwa Mbunge katika Bunge la Jumuiya ni awe ni raia wa nchi mwanachama

na awe na sifa ya kuchaguliwa kuwa mbunge katika nchi yake kulingana na sheria na taratibu za nchi hiyo.

Hata hivyo, Wabunge wa EALA si wabunge wa vyama, wala EALA si bunge la kupiga siasa. Nchi majirani zetu, hutangaza nafasi hizi, raia wake huziomba si kupitia vyama, ili kupata watu wenye uwezo.

Kwa Tanzania, nafasi hizi hugombewa kupitia vyama. Kwa nafasi yangu ya mwandishi wa habari, nimekuwa nikihudhuria vikao vya Bunge hili na ukiangalia jinsi wabunge wa nchi za wenzetu wanavyochangia mada na mijadala, ulinganishe ni michango ya wabunge wa Tanzania, kusema ukweli, ukiondoa wabunge wawili watatu waliokuwa 'active' mle, kiukweli kabisa katika EALA iliyopita, Tanzania tulipeleka majanga!.

Katika uchaguzi wa wabunge wa EALA mwaka huu, nikatoa ushauri wa jinsi ya kupata watu mahiri. Kwanza, kwa waliokuwa wawakilishi wetu kwenye Bunge hilo ambao wanataka kuwania kuendelea kwa awamu ya pili, waulizwe katika uwakilishi wao, kwa miaka 5 iliyopita, wamechangia nini na wamelisaidia nini taifa?. Hili ndilo swali la Mbunge wa Geita Vijijini (CCM), Joseph Msukuma aliuliza kwa mmoja wa wagombea.

Ushauri wa pili, wagombea watengeneze ajenda za Tanzania kama nchi wanazotaka kwenda kuzipigania kwenye EALA na kupewa dakika tano za kujieleza kwa lugha ya Kiingereza safi kilichonyooka!. Moja ya sababu za baadhi ya wawakilishi wetu kuwa mabubu kwenye mijadala ya kuchangia hoja za Bunge la Afrika Mashariki ni lugha.

Bunge letu limeweka uwiano wa wabunge wanane kutoka CCM na mmoja wa upinzani. CCM iliteua majina manane kwenda kupigiwa kura bungeni! Yaani nafasi ni nane CCM ikateua majina manane kupigiwa kura na wabunge! Katika hili hebu tuambiane ukweli, Bunge lilikuwa linachagua au ni kiini macho tu cha kuthibitisha chaguo la CCM?.

Kwa maoni yangu, kiukweli kabisa, CCM imelikosea sana Bunge letu kulipatia wanachama wanane kwa ajili ya kuwathibitisha tu. Uchaguzi wa wabunge wa EALA uliofanywa na Bunge letu, ni wabunge wetu wamefanya uchaguzi wa kumchagua mbunge mmoja tu wa upinzani na kuwathibitisha wabunge wanane wa chaguo la CCM.

Kufanya kosa si kosa!, kosa ni kurudia kosa. Kama mwanzo tulipeleka majanga EALA, halafu tukarudia makosa yale yale, unategemea nini?. Tena hapa naomba kutoka pongezi kwa Mbunge Dk. Musukuma, swali lake ambalo ndilo limeliokoa Bunge letu.

Tanzania ni nchi yetu sote, ni mali ya Watanzania wote wa vyama vyote. Kunapokuja kwenye masuala makini na muhimu kama kuchangua wawakilishi wa nchi, tulipaswa tuweke pembeni siasa za vyama na kutanguliza mbele maslahi mapana ya taifa.

**Mungu Ibariki Tanzania.**
**Wasalaam**
**Paskali 0754 270403**
**pascomayalla@gmail.com**

MADONGO YA MGAGAGIGIKOKO

# Bima ya afya isijadiliwe kama tozo!



Na Joseph Kulangwa

Ili kuhakikisha Watanzania Bara wanapata huduma bora ya afya kwa wote, serikali hivi karibuni iliwasilisha bungeni Muswada wa Bima ya Afya kwa Wote, ukasomwa kwa mara ya kwanza.

Muswada huo unaotarajiwa kupitishwa kuwa sheria Novemba, mwaka huu, ulisubiriwa kwa hamu na ghamu na Watanzania hao kwa kipindi kirefu kutokana na mpango uliopo kuonekana kudorora.

Kudorora huko kulikuja kuthibitishwa pia na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) katika ukaguzi wake wa 2021/22 alipogundua madudu mengi ya udanganyifu, yakiwamo ya wanaume kupata mimba na kufanyiwa upasuaji!

Lakini pia ni mahitaji ya Watanzania kuwa na bima ya afya kutokana na ukweli kuwa gharama za matibabu ziko juu lakini pia wimbi la magonjwa limekuwa kubwa na kuna kuibuka magonjwa ya aina mbalimbali kila kukicha.

Yote hayo yanaendana na ukata unaowakabili Watanzania hao, ambao idadi kubwa hawana ajira na kama wanayo ni ya wasiwasi na kipato chao ni cha kijungujiko, hivyo kushindwa kutoa kipaumbele kwenye matibabu bali matumbo.

Serikali kuja na muswada huu unaotarajiwa kuwa sheria, yawezekana kuja kuwa mkombozi au mwangamizi. Hiyo itatokana na jinsi wabunge wetu waheshimiwa, watakavyokaa na kujadili lakini pia kuchambua muswada huo kwa kuzingatia hali halisi ya nchi na watu wake.

Wabunge watakapoujadili na kuchukulia kana kwamba Watanzania wote ni wabunge, kwa maana ya kipato, basi watarajie mpango huo kugonga mwamba muda mfupi baada ya kuanza kutumika kwani Watanzania wengi huenda wakakwama kuchangia.

Watakapokuwa wanaujadili, watilie maanani kwamba Mtanzania wa leo (si wote, lakini wengi) yupo kwa ajili ya kula zaidi na si kujenga au kununua vyombo vya moto. Hiyo ni kutokana na hali halisi ya kipato na hali halisi ya uchumi wa mtu mmoja mmoja.

Hivyo, watakapofika kwenye kifungu cha nani achangie nini na kwa kiasi gani, hapo ndipo wakodoe macho na kubungua bongo zao ili waje na viwango rafiki kwa mtu wa kawaida ambao ndio wengi katika nchi hii aliyotuachia Nyerere.

Kuna mahali muswada unatamka kuwa aliye kwenye ajira, atakatwa asilimia sita ya mshahara huku kiwango kinachosalia kikilipwa na mwajiri kiasi cha nusu au zaidi ya hapo lakini wale hohehahe, utatafutwa utaratibu wa jinsi ya kuwasaidia kumudu michango hiyo. Binafsi najiuliza, kama bima hii ni kwa wote, hivi nchi tajiri Tanzania, yenye rasilimali nyingi za madini, wanyama, maziwa, mito, miti, mabonde na milima, kama ambavyo tumekuwa tukiambiwa, haiwezi kuja na utaratibu rahisi tu?

Kwamba, haya kila Mtanzania kila mwisho wa mwezi achangie angalau Sh 5,000 au Sh 10,000 na kiasi kingine achangiwe kutokana na tanzanite, almasi, dhahabu, nyumbu, nyati, tembo, simba, mitiki na mikaratusi. Kweli tutashindwa kutibiwa bila ubaguzi?

Hapa sasa ndipo ufike wakati wa kuthibitisha zile kauli za "Tanzania ni nchi tajiri na miradi yote tunaitekeleza kwa fedha zetu za ndani" ili wananchi wanufaike na keki yao hii badala ya kupakana mafuta kwa mgongo wa chupa.

Mimi kwa heshima zote kwa waheshimiwa wetu wabunge, watulie wajadili hili la bima kwa umakini mkubwa na kuja na jambo la kututia moyo sisi hususan walalahoi. Isiwe kama walivyojadili na kushadidia tozo, hatimaye zikaja kututokea puani na ghafla tukaanza kusukumiana mzigo wa nani mwasisi!

Lakini lingine, ni hili la masharti ya kujiunga na bima ya afya kwa wote ambayo upande mmoja tunaambiwa ni wa hiari, lakini tukichungulia upande wa pili tunaona kaulazimalazima hivi.

Kwa mfano hebu tuangalie hapa, Ibara ya 32, inasema: "Kwa kuzingatia sheria zilizotungwa na Bunge, mamlaka zinazohusika na usimamizi au utoaji wa leseni ya udereva, bima ya vyombo vya moto.

"Utambulisho wa mlipa kodi, usajili wa laini za simu, leseni ya biashara au hati ya kusafiria au viza, uandikishaji wa wanafunzi wa kidato cha tano, kidato cha sita na vyuoni, na utoaji wa kitambulisho cha Taifa.

"Zitahakikisha kuwa usajili au utoaji wa vibali, hati au leseni kwa waombaji unazingatia kigezo cha uwepo wa uthibitisho wa uanachama katika skimu ya bima ya afya." Hivi hatuoni haya ni mambo muhimu na ya msingi sana kwa maisha na mustakabali wetu mpaka yawekewe masharti kama haya? Tutafakari kabla ya kuamua. Alamsiki!

***kulangwasos@gmail.com**

# Waziri abaini tatizo kwa ma-DED, watendaji ardhi

**Na Waandishi Wetu,** DODOMA

WAZIRI wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Dk. Angeline Mabula amewataka wakurugenzi wa halmashauri nchini kujipanga na kufanya kazi kwa pamoja na wataalamu wa ardhi ili kuondoa shida zinazojitokeza katika utendaji kazi na usimamizi wa sekta ya ardhi katika halmashauri.

Dk. Mabula aliagiza hayo jana wakati wa ufunguzi wa kikao kazi kilichowaunganisha wakurugenzi wa halmashauri na wataalamu wa Sekta ya Ardhi nchini kilichofanyika jijini Dodoma.

Kikao hicho kilifanyika kwa lengo la kupata maoni kuhusu muundo mpya wa utendaji kazi wa wataalamu wa ardhi katika ngazi ya halmashauri.

Dk. Mabula alisema zimeanza kujitokeza shida katika utendaji kazi kati ya watendaji wa sekta ya ardhi na wakurugenzi wa halmashauri, hasa katika eneo la usimamizi wa sekta hiyo baada ya kuanza utekelezaji wa rejesho la Waraka wa Utumishi Na. 1 wa Mwaka 1998 kuhusu usimamizi wa watumishi wa sekta ya ardhi na maji kutokana na sababu mbalimbali.

Rejesho hilo pamoja na mambo mengine liliwahamisha wataalamu wa sekta ya ardhi kutoka kwenye usimamizi wa mamlaka za serikali za mitaa kiajira na kinidhamu na kuwa chini ya usimamizi wa Wizara ya Ardhi.

"Watumishi hawa kiajira na kinidhamu wako Wizara ya Ardhi, mamlaka za upangaji ardhi ziko halmashauri lakini baadhi ya wakurugenzi wamekuwa wakijiweka mbali na wataalamu ardhi na kushindwa kufuatilia utekelezaji wa sekta ya ardhi au kukosa ufahamu katika sekta ya ardhi," Dk. Mabula alifafanua. Kwa mujibu wa waziri huyo, suala hilo limeleta mkanganyiko kwa kuwa baadhi ya watendaji, hasa wakurugenzi, hawaoni kama wana wajibu wa kusimamia sekta ya ardhi wakati wao ni mamlaka za upangaji ardhi.

"Baadhi ya wakurugenzi hawajui taratibu za ardhi na kutojihusisha zaidi na uelewa wa masuala ya ardhi kwani unakuta Mkurugenzi wa Halmashauri ukimtaka akupe taarifa anakimbilia kupata ufafanuzi kutoka kwa mtaalamu wa ardhi," alisema.

Shida nyingine iliyoainishwa na Dk. Mabula ni kitendo cha baadhi ya wakurugenzi wa halmashauri kushindwa kurejesha fedha za mkopo wa Programu ya Kupanga, Kupima na Kumilikisha Ardhi na kutumia fedha hizo kwenye mipango mengine badala ya kurejesha fedha hizo ili zitumike katika maeneo mengine.

Katibu Mkuu Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Dk. Allan Kijazi alieleza kupitia kikao hicho kuwa ipo haja kuboresha mawasiliano kati ya watendaji wa sekta ya ardhi na mamlaka za serikali za mitaa ili kuweka mkakati mzuri wa utendaji kazi kwa kuwa wote ni watumishi wa serikali.

Dk. Kijazi alisema kumekuwa na tatizo la kiutendaji kati ya serikali za mitaa na uongozi wa kisiasa ikiwamo madiwani na kusisitiza kuwa jambo la msingi ni kufanya kazi kwa pamoja kwa kuwa wote ni watendaji wa serikali.

"Lengo la kikao chetu ni namna ya kuboresha mawasiliano ili tuweze kujiweka sawa kuboresha utendaji kazi kwani kumekuwapo lugha zinazoleta sintofahamu kuwa baadhi ya wakurugenzi wa halmashauri wamekuwa wakitoa kauli kuwa watendaji wa sekta ya ardhi wako chini ya Katibu Mkuu na wao hawahusiki," alisema Dk. Kijazi.

Madhumuni ya kikao kazi ni kujadili kero zinazojitokeza na kutoa maoni na ushauri kuhusu namna bora ya kusimamia watumishi wa sekta ya ardhi nchini kuwa na ufanisi na kwa maslahi mapana ya nchi.



Ofisa Mwandamizi wa Idara ya Rasilimali Watu wa Kampuni ya Geita Gold Mining (GGML), Innocent Mushi (wa pili kushoto) akitoa maelezo kwa Mkuu wa Wilaya ya Nyang'wale, Jamhuri William (wa pili kulia), kuhsu wanavyotoa fursa kwa wazawa kupata ajira na kushika nyadhifa za juu ndani ya kampuni hiyo, alipotembelea banda la GGML, ambao ndio wadhamini wakuu wa maonyesho ya kitaifa ya teknolojia ya madini, mkoani Geita. Kushoto ni Ofisa Mafunzo wa GGML, Egidius Mzale. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Watumishi TANESCO mbaroni kwa tuhuma kulihujumu shirika

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

WATUMISHI wawili wa Shirika la Umeme (TANESCO) wilayani Kahama wanashikiliwa na Jeshi la Polisi wilayani hapa kwa tuhuma za kuhujumu shirika hilo kwa kuiba mita mbovu na kuwafungia wateja mbalimbali na kusababisha hasara ya zaidi ya Sh. milioni 10.

Imedaiwa kuwa vitendo hivyo walikuwa wakivifanya kwa kushirikiana na mafundi vishoka ambao awali walikuwa wakifanya kazi ya kujitolea katika shirika hilo katika miradi mbalimbali ikiwamo ile ya upelekaji wa umeme maeneo ya vijijini.

Kaimu Meneja wa Shirika hilo, Tumain Chonya alibainisha hayo jana alipozungumza na vyombo vya habari, akisema kuwa kati ya Septemba 25 na 29 mwaka huu, walifanya operesheni ya ukaguzi wa mita za wateja wao na kubaini wengi wanatumia huduma kwa muda mrefu bila shirika kufahamu.

Alisema kuwa katika operesheni hiyo walikamata wateja 13 akiwamo kiongozi wa dini na wakazi wengine wanaopata huduma hiyo kwa njia ya undanganyifu, pia wakibaini mmoja wa watumishi wa shirika hilo alipatiwa Sh. 600,000 kinyume cha sheria ili kuwapa huduma ya umeme.

Chonya alisema watumishi hao kwa kushirikiana na mafundi vishoka walikuwa wakiiba vifaa mbalimbali vya TANESCO ndani ya stoo ya shirika na kwenda kuwafungia wateja na kujipatia fedha.

Meneja huyo alitaja baadhi ya vifaa vya umeme vilivyoibwa na kufungiwa wateja hao kuwa ni nyaya za shaba za mifumo ya ardhi inayofungwa kutoka kwenye transfoma hadi ardhini, mita mbovu, nyaya mbalimbali, kobe, mikanda ya kupandia nguzo za umeme na glovu, vyote vikiwa na thamani ya zaidi ya Sh. milioni 10.

Alisema mpaka sasa jumla ya transfoma 73 zimehujumiwa kwa kukatwa nyanya za shaba na kuhatarisha usalama wa miundombinu hiyo hasa wakati wa mvua za masika na zaida ya nyaya hizo 1,460 zimeondolewa na kuliingizia hasara shirika kuzirejesha.

"Nimesikitika sana kuona watumishi wangu wanakuwa sehemu ya watu wasiokuwa na uadilifu kuhujumu miundombinu ya shirika, polisi wanaendelea na upelelezi wao na pale watakapokamilisha watafikishwa mahakamani kujibu tuhuma zinazowakabili," alisema.

Chonya aliwataka wananchi wote kutoa taarifa kwa TANESCO na Jeshi la Polisi wanapoona tangu wamefungiwa huduma hajawahi kulipia huduma kwa kuwa wakikamatwa, watashtakiwa kwa jinai ya uhujumu uchumi.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Shinyanga, Janeth Magomi alithibitisha kukamatwa kwa watumishi hao ambao hakutaka kuwataja majina yao ili kutoharibu upelelezi.

Alisema kuwa katika operesheni hiyo walikamatwa watuhumiwa 13. Kati yao, mafundi vishoka ni wanne, watumishi wa shirika hilo wawili na wateja saba waliounganishiwa huduma kwa njia ya udanganyifu na wote watafikishwa mahakamani wakati wowote.

## UN yatoa tuzo 2 kwa Rais Samia

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

RAIS Samia Suluhu Hassan ametangazwa mshindi wa tuzo mbili za Rais, ya Dhahabu ya Malengo ya Maendeleo Endelevu (SDG) na Amani ya Dunia 2022 zinazotolewa na Umoja wa Mataifa (UN).

Kutokana na ushindi huo, Umoja wa Wanawake wa Tanzania wa Chama Cha Mapinduzi (UWT), umetoa tamko la kumpongeza huku ukitaja maeneo mbalimbali yaliyompa sifa ya kushinda tuzo hizo ikiwamo kujali usawa wa kijinsia.

Akizungumza jana na waandishi wa habari jijini hapa, Mwenyekiti wa UWT Taifa, Gaudentia Kabaka, alisema Rais Samia alitangazwa mshindi wa tuzo hizo na UN kupitia Kurugenzi ya Jumuiya ya Kimataifa ya Watetezi wa Amani wiki iliyopita na atakabidhiwa Oktoba 24 mwaka huu.

"Tuzo hizi amezipata kutokana na juhudi zake katika ujenzi, uboreshaji wa miundombinu ya afya elimu ndani ya kipindi kifupi, pia amekuwa championi wa amani kwa kuhakikisha kuna uhuru wa kuabudu lakini amesamehe wafungwa wa kisiasa na kuweka mazingira ya karibu zaidi na vyama vya upinzani.

"Amekuwa Rais wa kwanza mwanamke Afrika kupatiwa tuzo hizi, sisi UWT na wanawake wa Tanzania tumeona fahari sana kuwa na Rais mwanamke, kwa Afrika waliowahi kuzipokea hizi tuzo ni Rais George Weah wa Liberia na Rais Seretse Ian Khamu wa Botswana," alisema.

Alifafanua kuwa kurugenzi hiyo ya kimataifa imemtambua Rais Samia kwa kuteua wanawake wengi kushika nafasi mbalimbali ambapo Tanzania inaongoza katika Bara la Afrika.

"Rais amefanikisha suala la usawa kwa kuteua wanawake wengi wakuu wa wilaya, wakuu wa mikoa, makatibu tawala wa mikoa na wilaya, wakurugenzi, makatibu wakuu wa wizara, mawaziri na wenyeviti wa bodi mbalimbali.

"Kwenye tuzo ya maendeleo endelevu ambayo kurugenzi imeangalia zaidi lengo namba tatu la afya njema na ustawi wa jamii, lengo la nne la utoaji elimu bora ambapo Rais Samia amejenga madarasa ya kutosha kwa shule za msingi na sekondari na kutoa elimu bila ada," alisema.

Kabaka alisema UWT inatambua jitihada za Rais na wanaamini suala la usawa wa kijinsia litafika 50 kwa 50 ifikapo mwaka 2030.

MAISHA
OKTOBA 2, 2022
Nipashe
Baba, Mama na Mwana
Jumapili



Ukurasa 15

## Yajue magonjwa yanayoathiri nyumba, uyaepuke



Ukurasa 14

## Jinsi ya kupika dagaa haraka



## VIZIBAO VINATOSHA Kukung'arisha msimu wa joto


Ukurasa 13


# Jaza nywele kwa njia asili



Ukurasa 14

## MAJIBU YA WIKI ILIYOPITA






| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| ■ | D | I | M | B | A |
| ■ | O | ■ | ■ | A | ■ |
| O | N | A | ■ | M | ■ |
| ■ | Y | ■ | I | B | A |
| ■ | O | ■ | ■ | I | ■ |
| Y | A | N | G | A | ■ |

## AMSHA AKILI

TUMIA RANGI YA NJANO NA KIJANI



## TOA TOFAUTI 5



## FUMBO TOTO

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| ■ | | | | | |
| ■ | | ■ | ■ | | ■ |
| | | | ■ | | ■ |
| ■ | | ■ | | | |
| ■ | | ■ | ■ | | ■ |
| | | | | | ■ |

Jaza maneno yafuatayo katika vyumba vilivyopo wazi:
ANA, BEI, TENGA, KWETU, TWANGA, KWENYE

## WATOTO

# PAKA RANGI







MTOTO Grace alikuwa akimsaidia mama yake kuchuma matunda ya nanasi shambani. Wakati wakiendelea na kazi hiyo alimuuliza mama yake kuhusu namna ya uchumaji wa matunda hayo.

Grace: Eti mama tunavyochuma mananasi hapa juani ni lazima yaliwe kivulini?

Mama: Hapana matunda huliwa sehemu yoyote, lakini ni vyema kula wakati umetulia na hasa kivulini ambako hakuna jua.

Grace: Kwa maana hiyo mwalimu alikosea alituambia mchumia juani hulia kivulini?

Mama: Huo ni msemo tu mwanangu, unamaanisha kwamba kila anayetafuta kwa tabu hupata mafanikio baadae na hapo hupata raha na sivyo kama wanavyodhani.

SWALI

Matunda ya zabibu yanazalishwa katika mkoa gani wa Tanzania?

## MAISHA NDIVYO YALIVYO
Na Flora Wingia



# Amdharau mamaye akiwa daktari, akaishia kuishi na kula jalalani !

KARIBU tena msomaji wangu tuendelee na ujumbe kwa wale wanaowadharau au kuwasahau wazazi wao, pale wanapofanikiwa kimaendeleo.

Wiki iliyopita nilieleza kwamba kuwadharau wazazi wako ni laana mbaya sana unayoitengeneza mbele yako, na hakika haitakuacha salama. Ndiyo maana Mungu akasema mapema kwenye moja ya maandiko yake kwamba: "Na alaaniwe amdharauye baba yake au mama yake. Na watu wote waseme, Amina".(Kumb. 27: 16).

Nilitoa mfano wa dada mmoja aliyemshupalia mama yake mzazi kwamba analoga watoto wake (wajukuu), jambo ambalo mama alikanusha hata mbele ya viongozi wa kijiji.

Lakini binti alipoweka msisitizo, mama akaona isiwe taabu, akajiua kwa kunywa sumu. Tokea hapo binti huyo anazurura na watoto wake miji mbalimbali kuomba msaada. Laana ya mama yake haijamwachia hadi leo!

Msomaji wangu, hebu sasa sikiliza kisa kingine cha kutisha cha binti daktari aliyeishia kuishi na kula jalalani, kisa alimdharau mama yake ambaye naye alikufa kwa ghadhabu.

Kisa hiki kipo hivi, dada mmoja alikuwa akiishi na wazazi wake. Baada ya kufikisha umri wa miaka saba, baba yake mzazi alifariki dunia. Mama yake pale kijijini akaendelea kuishi maisha ya taabu sana.

Ndugu zake wakamshauri kuwa maadam bado ni msichana kwa nini asiolewe tena ili amtunze huyo mtoto. Yeye akasema hawezi kuoelewa ila anatamani amsomeshe mwanawe ili atimize ndoto zake.

Mama akawa anafanya vibarua mbalimbali kama vile kufua nguo za watu, kuuza mboga ili mradi apate fedha ya kula na kumsomesha binti yake.

Binti akasoma naye alikuwa na akili sana darasani. Akasoma hadi akamaliza darasa la saba na kufaulu akachaguliwa kuingia kidato cha kwanza. Mama akawaza atafanya nini aendelee kumsomesha kwa kuwa hana biashara na yuko kijijini.

Huku akiendelea kumwomba Mungu juu ya suala hilo, Mungu naye akatenda muujiza.

Huko serikalini ikatangazwa kuwa wanahitajika watoto wanaoishi kwenye mazingira magumu ambao wazazi wao hawana uwezo au wale ambao wameondokewa na wazazi wao ili wasaidiwe kwa kuwa wamepatikana wafadhili, hivyo wanahitaji watoto 10 kwenye kijiji chao.

Bahati nzuri Mwenyekiti wa Serikali ya Mtaa wao akaandika pia jina ya yule binti, akachukuliwa na wafadhili na kupelekwa shule ya bweni ya wasichana. Huko akasoma vizuri kwa sababu alikuwa na akili tangu akiwa mdogo.

Aliendelea kufanya vizuri kwenye masomo hadi akamaliza kidato cha nne. Napo akafanya vizuri na kufanikiwa kujiunga na kidato cha tano na cha sita. Huko akafanya pia vizuri akachaguliwa kujiunga chuo kikuu kwa masomo ya udaktari.

Alichukua masomo ya udaktari, akasoma miaka mitano na kumaliza. Lakini cha ajabu ni kwamba huyu binti tokea amepelekwa na hao wafadhili, hakuwahi kurudi tena nyumbani.

Je, unaweza kusema kuwa hajui njia au aliondoka akiwa mdogo sana? Hivi binti aliyemaliza darasa la saba na kuingia kidato cha kwanza ni mdogo kusahau kwao? Anajua ila aliamua tu kuendelea na maisha yake.

Kutokana na hali hiyo, alimsahau mama yake aliyejinyima akasema sitaolewa ili nimtunze binti yangu. Akawa anashangaa kapotelea wapi, au amekufa anafichwa?

Mama akafadhaika akawa anajiuliza labda hawa viongozi wa serikali ya mtaa wananificha pangine binti yangu hayupo. Lakini walimtia moyo kwamba hajambo.

Binti akaendelea na kumaliza chuo kikuu na kupata nafasi nzuri ya kuwa daktari kwenye hospitali kubwa hapa nchini. Akaendelea kufanya kazi akabadilishwa jina na kuitwa daktari fulani (jina linatajwa).

Marafiki zake anawaambia kwamba hana baba wala sina mama, hana kaka wala dada. Fedha zake zote alikula na marafiki zake.

Akapewa nyumba nzuri ya kifahari na gari la kutembelea kwani ni daktari mkubwa. Lakini hizi fahari zote zinaishia kwa rafiki zake. Alishasema hana wazazi wala ndugu lakini ukweli ni kwamba mama yake alikuwapo kule kijijini.

Kutokana na kufikia kiwango hicho cha mafanikio, anaona kuwa mama yake si wa hadhi yake. Anasahau mama alivyofanya vibarua ili asome lakini leo hamjui.

Tuishie hapa, wiki ijayo tutaona yaliyomkuta binti na mamaye. Je, una maoni, kisa? Ujumbe 0715268581.

## NAWAZA KWA SAUTI
Na Salome Kitomari



# Jamii ichukue hatua ongezeko la ubakaji, ulawiti

MATUKIO ya ulawiti na ubakaji kwa watoto yanaongezeka kila uchao huku kesi nyingi zinaelezwa kuishia polisi au mtuhumiwa anapopewa dhamana familia zinakaa kuzungumza ili kuyamaliza kifamilia.

Pia baadhi ya vijana waendesha bodaboda wanadaiwa kuhusika na matukio hayo hasa wale wanaowabeba wanafunzi kuwapeleka na kuwarudisha shuleni kiasi kwamba wako watoto wamefanyiwa ukatili na kuuzoea au kulazimishwa kuishi maisha ya mateso tangu wakiwa wadogo.

Kwenye shule za msingi na sekondari matukio hayo yanaongezeka kwa watoto kufanyiwa hivyo na ndugu wa karibu, ambao hulala nao wanapokaribishwa na mama, baba au mlezi anashtuka mtoto ameshaharibika.

Aidha, inadaiwa fedha inatumika kumaliza kesi hizo na wakati mwingine madawati ya jinsia yamelalamikiwa kuwa sehemu ya uharibifu ambao sasa ni maumivu kwa jamii.

Unapokwenda maeneo ya starehe utakutana na vijana wa kiume wa rika mbalimbali wanajiuza yaani wanaingiliwa kinyume cha maumbile na wanaume wenzao, huku wasichana wakiwa na uhusiano na wasichana au wanawake wenzao.

Vitendo hivi vinaua kizazi kwa kuwa idadi ya wanaume inaendelea kupungua kila siku, huku takwimu zilizopo zikionyesha wanaume ni wachache ikilinganishwa na wanawake, sasa linapotokea suala la ulawiti linapunguza idadi yao na kukiweka kizazi hatarini.

Inaelezwa kuwa mwanamume anapofanyiwa kitendo hicho, anatamani kuendelea kufanyiwa ndiyo maana wengi hujiuza ili kupata wa kuwafanyia hivyo. Hili ni kosa kisheria na limekatazwa na kulaaniwa kwenye vitabu vitakatifu vya dini.

Utafiti mdogo uliofanywa na Ofisi ya Taifa ya Mshataka, ulibaini kuwa baadhi ya watuhumiwa wa makosa hayo wakiwa nje kwa dhamana, wanakimbia na wengine kuharibu ushahidi au kumalizana na wazazi au ndugu wa mwathirika wa vitendo hivyo.

Aidha, Kaimu Mkurugenzi wa Huduma za Sheria kutoka Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, Happy Msimbe, hivi karibuni alisema wizara imeanza mchakato wa kufanyia marekebisho Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai na wanaanza mchakato wa makosa ya ubakaji na ulawiti kuondolewa dhamana.

Katika kuonyesha ukubwa wa tatizo, takwimu za Jeshi la Polisi Tanzania katika kipindi cha Januari hadi Desemba, 2021, matukio ya ukatili kwa watoto yaliyoripotiwa ni 11,499 huku makosa yaliyoongoza kwa idadi kubwa ni ubakaji (5,899), mimba kwa wanafunzi (1,677) na ulawiti (1,114).

Aidha, mikoa iliyoongoza kwa matukio ya ukatili na idadi kwenye mabano ni Arusha (808), Tanga (691), Shinyanga (505), Mwanza (500) na mkoa wa kipolisi Ilala (489).

Baadhi ya familia zinamaliza kesi hizo nyumbani na inapotokea mzazi mmoja anashikilia kuendelea na kesi mahakamani anaitwa na kukalishwa na ukoo, ikiwamo kutengwa kama atakubali kuendelea na kesi.

Wengi wanaokumbwa na kesi hizi wanatoka familia maskini ambazo wakati mwingine kufuatilia kesi ni usumbufu na gharama. Wakati mwingine wanakutana na usumbufu mkubwa polisi na hospitalini, hivyo kuamua kubaki nalo moyoni.

Wanaoteseka ni watoto na wazazi wao ambao wametendewa ukatili huo, lakini hawana pa kukimbilia kwa kuwa kila eneo hakuna msaada na mwisho matukio huendelea kutokea.

Mabadiliko ya sheria hiyo kuongeza makali ni hatua nzuri sana kwa kuwa watu wataogopa na kesi zitashughulikuwa inavyotakiwa kwa kuwa ushahidi hautaharibiwa kama inavyofanyika sasa.

Ni muhimu kulinda taifa dhidi ya ongezeko la mashoga ambao wanakuwa hivyo siyo kwa msukumo wa maumbile, bali kwa kufanyiwa ukatili na wachache ambao wananufaika au ni tamaa za mwili.

Lakini ni muhimu kuendelea kutoa elimu na kuchukua hatua mapema taarifa zinapotolewa, kuboresha madawati ya jinsia ili yasiwe kichaka cha rushwa na kumiza watu, viongozi wa dini walio waadilifu kuendelea kuwahubiri yaliyomema waumini wao na kuwaonya kwa kutumia maandiko matakatifu juu ya vitendo hivyo.

Sheria kufanyiwa mabadiliko ni jambo jema lakini bila kudhibiti rushwa ni sawa na bure kwa kuwa watu wataendelea kufinyanga kesi za namna hiyo, ili kupata fedha kwa waliotenda pasipo kuona uharibifu huo ipo siku utabisha hodi kwenye nyumba yake.

Kwa sasa tuna Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Makundi Maalum, ambayo imeunda kamati mbalimbali kukabili vitendo vya ukatili, lakini ni muhimu kufuatilia hadi ngazi ya chini hasa kwenye shule za msingi na sekondari, lakini pia kuimarisha idara ya ustawi wa jamii, polisi na hospitali ili wafanye kazi kwa hofu ya Mungu na kuogopa kuyaharibu matukio hayo.









Ilikuwa siku ya furaha kwa ndugu na jamaa wa Theresia Karagea wakati walipomuaga na kumpa baraka zao kwenda kufunga ndoa na Pascal Kitomari. Sherehe hiyo ilifanyika Septemba 15, katika ukumbi wa Flamingo ulioko Mbezi Beach, Dar es Salaam.

## MITINDO



# VIZIBAO VINATOSHA
## Kukung'arisha msimu wa joto



VIZIBAO ni moja ya mavazi ya kawaida ambayo yana umaarufu kutokana na kupendwa na watu wengi.

Kuna aina nyingi za nguo za kiume, basi mtindo huu wa mavazi usiuweke kando kwani una ladha tofauti katika kupangilia mavazi yako.

Kwa mfano vizibao aina ya Puffer ni nyongeza nzuri kwa hafla yoyote ikiwa katika hali ya hewa ya joto au baridi.

Nguo hizi zimetengenezwa zikiwa laini chini, na kukupa mwonekano mzuri unapovaa na aina yoyote ya mavazi.

Ikiwa katika hali ya joto nguo ya aina hii, inakuruhusu mwili wako kupumua vyema.

Aina nyingine ni ile ya Suede, ambayo huvaliwa zaidi mahali pa kazi na matukio mengine ya kitaaluma, hata hivyo daima hukuweka tofauti.

Inapendekezwa kuunganisha na fulana au shati maridadi na chini pigilia suruali.



URENBO

**Na Mary Geofrey**

# Jaza nywele kwa njia asili



NYWELE ni moja ya sehemu ya urembo kwa wanawake na kuongeza utanashati kwa wanaume.

Kila mtu anapenda awe na nywele nzuri, ndefu na zenye afya.

Kuna wale ambao wana nywele hazirefuki lakini pia ni chache.

Kwa wenye tatizo hilo hii ni fursa kwao kujifunza siku ya leo namna unaweza kutumia matunda na asali kurefusha nywele zako.

Unaweza ukawa na nywele ndefu zisizokatika na zilizojaa kichwani kwa kufanya mambo nitakayoyaeleza hapa.

Chukua parachichi kubwa moja, asali vijiko vitatu na kiini cha yai.

Osha nywele zako kwa shampoo na kisha uzikaushe.

Ponda ponda parachichi mpaka lilainike kabisa. Chukua vijiko vitatu vya asali na kiini cha yai kisha changanya vyote kwa pamoja.

Paka mchanganyiko huo kaa nao kwa muda wa dakika 15 kisha osha.

Fanya hivyo kwa muda wa wiki moja hadi mbili na utaweza kuona matokeo mazuri katika nywele zako.

Mwisho

MAPISHI

**Na Mary Geofrey**

# Jinsi ya kupika dagaa haraka

KUPIKA dagaa unahitaji kuwa na nyanya, vitunguu, swaumu, karoti, hoho na mafuta ya kupikia.

Dagaa tunazopika ni zile ambazo wengi tunapenda kuziita 'dagaa mchanga' au dagaa wa Mwanza.

Katika mapishi ya mboga yetu hii tunahitaji viungo vichache tu kwa sababu tunapika ili siku nyingine upike nyingi.

**Namna ya kuandaa**

Anza kwa kukata kata vichwa vya dagaa, wengine huwa mnaunga dagaa bila kukata vichwa ni sawa pia ila ni vizuri kuondoa vichwa kwa sababu inasaidia kupunguza mchanga.

Baada ya hapo, bandika maji kidogo jikoni kwa ajili ya kuoshea dagaa, wakati maji yakiwa jikoni, saga nyanya zako vizuri, andaa hoho, kitunguu maji na karoti kwa kuzikata kata kwa mtindo mzuri kisha menya vitunguu swaumu punje tatu na uvitwange.

Unaweza kuongeza tangawizi kama utahitaji.

Sasa weka maji ya moto pembeni uliyoweka ukisubiri yawe ya uvuguvugu. Baada ya hapo osha dagaa kwa maji hayo vizuri na uzisuuze na maji ya baridi, lengo ni dagaa wawe safi lakini pia zisivunjike vunjike.

Hapa tunaanza na kuinjika sufuria yenye mafuta ya kupikia jikoni weka kitunguu maji na ukikaange mpaka kiwe cha kahawia kisha weka dagaa zako ulizoziandaa na uzikaange kwa muda wa dakika moja.

Baada ya hapo weka kitunguu swaumu kisha ukoroge kukichanganya kwenye dagaa zako.

Weka nyanya ulizosaga kwenye dagaa na uziache mpaka ziive kabisa.

Weka karoti ulizozikatakata kisha koroga kuzichanganya na mchanganyiko wako wa mwanzo.

Baada ya hapo weka maji robo ya kikombe cha chai na kisha weka pilipili ili upate harufu nzuri kwenye mboga yako.

Kabla haujafunika mboga yako, kamulia kipande cha limao kisha uweke chumvi kiasi na ufunike mboga yako kwa muda wa dakika nne hadi tano ili viungo viive vizuri.

Baada ya hapo dagaa zako ziko tayari kwa kuliwa na ugali na mboga ya majani pembeni.



MAISHA NI NYUMBA

**Na Elizabeth Zaya**



# Yajue magonjwa yanayoathiri nyumba, uyaepuke

KAMA ilivyo kwa viumbe hai kuathiriwa na mazingira wanayoishi, ndivyo ilivyo pia kwa viumbe visivyo hai ikiwamo nyumba.

Ili kuepuka majengo yasiathirike, ni vyema ubunifu ufanyike katika hali ya ubora wa hali ya juu katika sehemu husika linapojengwa jengo.

Msanifu Majengo, Deodatus Kwivilo, anasema hata ujenge nyumba nzuri na kubwa kiasi gani, kama haijabuniwa na kujengwa kwa kuzingatia mazingira ya eneo husika, lazima iwe hatarini kuathirika.

Kwivilo anasema kabla ya kuanza kujenga nyumba, ni lazima ufanye uchunguzi katika eneo husika kubaini kama kuna magonjwa yanayoweza kuathiri nyumba yako na kufanya ubunifu wa kukabiliana nayo.

Mtaalam huyo anasema endapo nyumba hiyo itajengwa pasipo kufanyiwa ubunifu mzuri, huenda ikaathiriwa na magonjwa hayo.

Anasema miongoni mwa magonjwa yanayoathiri nyumba endapo haijafanyiwa ubunifu mzuri ni kutitia kutokana na aina tofauti za udongo, kiwanja au kimo cha msawazo wa msingi kuwa tofauti pamoja na ubunifu hafifu wa udongo kulingana na uzito wa jengo husika.

Ugonjwa mwingine anasema ni nyumba kupitisha maji na kwamba maeneo mengi ya Tanzania yamezungukwa na vyanzo vya maji ambayo yanahitaji usanifu na ubunifu wa hali ya juu wakati wa ujenzi ili kuepuka athari baadaye.

"Maeneo mengi ya Pwani majengo yake mengi yameathiriwa na tatizo hili na hata limekuwa kero kwa wakazi na watumiaji wa majengo hayo. Baadhi ya majengo yanapitisha maji kwa njia ya sakafu na kuta mithili ya chujio au chemchemu na mara nyingi utagundua kwa kuona ardhi yake inatoa maji wakati wote wa majira ya mwaka.

" Na majengo mengi ya maeneo haya yanaoza na kutitia kwa haraka na hata mashimo ya vyoo vyake huinuka kwenda juu jambo ambalo ni hatari kwa afya za wakazi. Katika hali hii kuta na sakafu huoza kwa haraka kutokana na maji yaliyoko chini ya ardhi kuwa na kemikali mbalimbali zilizoko kwenye maji hayo. Kwa hiyo katika mazingira haya lazima yatumike malighafi sahihi za kuzuia maji hasa wakati wa ujenzi," anasema.

Lingine anasema ni kuoza kwa nyumba na kwamba hali hiyo hutokana na unyevunyevu na kemikali mbalimbali kupitia maji kukaa kwa muda mrefu kwenye kuta na kuathiri ubora wa kuta hizo.

"Na hii husababisha kumea kwa mimea ambayo kusababisha ukungu wa kijani kwenye kuta ambao huzalisha fangasi mbalimbali wanaokula ukuta," anasema.



## Namna ya kufunga chandarua chumbani



WAKATI wa msimu wa baridi watu wengi hawapendi kutumia chandarua wakati wa kulala wakiamini hakuna mbu, lakini ukweli wakati wote hatari ya kuumwa na mbu ipo na kukusababishia ugonjwa wa malaria. Ikiwa wewe ni mmoja wa wale wanaougua kila mwaka na malaria kwa kuumwa na mbu wanaoingia nyumbani, tutakupa miongozo ya jumla namna a kufunga vyandarua kwa kuzingatia usalama.

Siku hizi kuna aina ya vyandarua unanunua ukiwa na kila kitu na itabaki uwezo wako wa kufunga tu.


1: Hakikisha unachagua aina unayoipenda ya vyandarua kulingana na chumba chako kilivyo, Hapa unatakiwa kuwa makini ili usipate chandarua kisicholingana na kitanda au mfumo wa chumba.

2: Hakikisha unachukua vipimo halisi, kuanzia sehemu ambayo unataka kufunga.

3: Kuna aina mbalimbali ya ufungaji wa chandarua, kuna ya kuning'niza na ile ya kutumia vyuma maalum, hivyo ni muhimu kufuata maelekezo.

4; Ukifahamu kwa nini unahitaji chandarua, itakuwa upeo wa kutumia vyema wakati wa kulala kwani haitakiwi kufunga sehemu ambayo inaweza kuachia na kukusababishia kuwa wazi.

# KATUNI


KATUNIKA KI'DOMOKRASIA
BY ABDUL KINGO - 2022
SMS - 0621 412 879
JUKWAANI
HIVI WEWE UNAVYOONA HUU UCHAGUZI UNAVYORUDIWA NTATOBOA?
'TOBO GANI?
JEMBE LANGU... MTOTO WA KIUME HASIFIWI UMBEA!
HATA AKIWA KARITHI KWA BABA'AKE?
NACHEKA KAMA MAZURI, WALIO-KALIA KITI WOTE WASIMAME WIMA TUANZE UPYA! WAMENUNAJEE!
MIMI NIMEZALIWA DAR, UTANAMBIA NINI WAKUJA?
MABIFU YENU YA MTAANI MSI-YALETE HUMU TAFADHALINI
KWA HIYO ULITAKA WAYALETE OFISINI KWAKO ILI UBURUDIKE PEKE YAKO?
NO SALENDA
SINA CHA KUKWAMBIA NILIYOKUKUTA UNAKAA KWENU NIMEJENGA HA HAAA
WEWE NINI ACHA MOTO UWAKE ILI TUWAWEKEE MALI ZAO MAHALA PEMA
NINGEKUKUBALIA LAKINI NAMUOGOPA MKEO AKIJUA ANAWEZA KUNIUA, LABDA UNIPE MILIONI MBILI TU!
HIZO NDIO GHARAMA ZOTE ZA MAZISHI AKISHAKUUA?
MKE WANGU ILI NDIO ENEO SAHIHI YALE MADAI YAKO YA TALAKA NIKILEWA ANZA KUDAI
TALAKA AU LAKI TISA DENI LA MAHALI!
*KINYUNYIZO CHA LEO...
...RAHA YA KUKIMBIZWA UWE NA MBIO

# Marekani yaionya Russia, yasema kamwe haitishwi

**WASHINGTON,** Marekani

RAIS wa Marekani, Joe Biden ameionya Russia kwamba Marekani haitotishwa na vitisho vya ovyo kutoka kwa kiongozi wa nchi hiyo.

Kauli ya Biden imetoka baada ya Rais wa Russia, Vladimir Putin kuyatwaa maeneo manne ya Ukraine.

Rais Putin alitoa tishio la jumla kutumia silaha za nyuklia kuyalinda maeneo hayo.

Alitangaza kwamba maeneo hayo yatasalia daima kama sehemu ya Russia.

Katibu mkuu wa jumuiya ya kujihami Nato, Jens Stoltenberg alitaja kutengwa kwa maeneo hayo kama uchochezi wa hali ya juu tangu kuzuka kwa vita hivyo.

Katika hotuba yake, kiongozi huyo wa Russia alidai kuwa raia wa Kherson, Zaporizhzhia, Luhansk na Donetsk wamepiga kura kutaka kujiunga na chimbuko lao.

Alikuwa anataja kura za kutafuta maoni zilizoandaliwa katika maeneo hayo katika siku za hivi karibuni, lakini Ukraine na mataifa ya magharibi zimeshutumu kura hiyo na kuiita ya uongo.

Lakini sehemu kubwa ya hotuba ya Putin ilitumika kuyashambulia mataifa ya magharibi.

Alisema Marekani iliidhinisha mkondo wa kutumia silaha za nyuklia dhidi ya Japan mwishoni mwa vita vya pili vya dunia katika kilichoonekana kuwa tishio.

Wiki iliyopita Putin alisema nchi yake ina silaha tofauti za uharibifu na itatumia njia zote zilizopo na kusisitiza haropoki kwa maneno pekee.

Rais Biden ameshutumu matamshi hayo na kuyaita ya ovyo na tishio kutoka kwa kiongozi huyo na kueleza Putin hawezi kuwatishia.

"Marekani na washirika wake hawatotishika," Biden alisema akiwa katika Ikulu ya White House.

Baadaye alimtumia ujumbe kiongozi wa Russia moja kwa moja akinyooshea kamera kidole chake.

" Marekani imejitayarisha na washirika wetu wa Nato, kulinda kila sehemu ya maeneo ya Nato," alisema akitaja jumuiya hiyo ya magharibi ya usalama.

"Bwana Putin, usinielewe vibaya ninachosema: kila inchi." Alisisitiza.

Muda mfupi baadaye, ofisa mkuu wa usalama wa taifa wa Biden, alisema wakati kuna nafasi ya Russia kutumia silaha za nyuklia, hakuonekani kuwa na tishio linalowezekana kutokea.

Ukraine imeidhinisha ombi jipya la kutaka kujiunga kwa haraka na Nato punde baada ya hotuba ya Putin.

Rais Volodymyr Zelensky alisema Ukraine kwa muda mrefu imekuwa mwanachama, japo sio kisheria, wa jumuiya hiyo ya usalama na kuishutumu Russia kwa kuchora upya mipaka yake kwa kutumia mauaji, tishio, udhalilishaji na uongo.

Katibu mkuu wa Nato, Stoltenberg alikuwa anasita kuhusishwa katika ombi hilo, akieleza kuwa uamuzi upo miongoni mwa wanachama 30 wa jumuiya hiyo.

"Wanachama wa jumuiya hiyo hawayatambui na wala hawatoyatambua maeneo yoyote yaliyotengwa kama sehemu ya Russia," Stoltenberg aliwaambia waandishi wa habari.

Korea Kusini imesema haitambui kutengwa kwa maeneo hayo, ikiongeza kuwa Uhuru wa Ukraine, usalama wa maeneo yake ni lazima ulindwe.

Wakati Putin akizungumza akiwa Moscow, vikosi vyake vilizungukwa na wanajeshi wa Ukraine katika eneo la Lyman, mji muhimu ulioko katika jimbo la mashariki la Donetsk kati ya maeneo yaliyotengwa na Russia.

Jeshi la Ukraine limekuwa likificha kasi ya wanajeshi wake katika eneo hilo, lakini video moja katika mtandao wa kijamii ilionekana kuonyesha vikosi vya nchi hiyo vikiwa katikati ya Yampil, takriban kilomita 16 kusini mashariki mwa Lyman.


Ijumaa jioni Wizara ya Ulinzi ya Ukraine, ilisema imedhibiti kijiji cha Drobysheve, kilomita 8 kaskazini magharibi mwa Lyman.

Kwengineko huko Zaporizhzhia takriban raia 30 wa Ukraine wameuawa katika shambulio la kombora la Russia dhidi ya msururu wa magari ya raia.

Wakati huo huo, Russia imepiga kura ya turufu dhidi ya azimio la baraza la usalama la Umoja wa mataifa lililoshutumu hatua yake ya kuyatenga maeneo manne ilioyakalia.

Balozi wa nchi hiyo, Vasily Nebenzia, alilalamika kwamba haikutarajiwa kushutumiwa kwa mwanachama wa kudumu wa baraza hilo.

**BBC**



Kikongwe akipita karibu na jengo lililoharibiwa na bomu la Russia huko Kramatorsk, mashariki mwa Ukraine jana.
PICHA: AFP

# Wabrazil kumchagua rais leo

**BRASILIA,** Brazil

KAMPENI za kuwania urais nchini Brazil zilikamilika jana huku kukishuhudiwa upinzani mkali kati ya rais wa sasa na mgombea kutoka kambi ya siasa kali za mrengo wa kulia Jair Bolsonaro na Luiz Lula Da Silva.

Da Silva ambaye anatoka kambi ya mrengo wa kushoto, pia aliwahi kuiongoza nchi hiyo kutoka mwaka 2003 hadi 2010.

Uchaguzi wa rais unafanyika leo huku nchi hiyo yenye uchumi mkubwa katika ukanda wa Amerika ya Kusini ikiwa imegawanyika.

Ili kupata ushindi mgombea atalazimika kupata zaidi ya asilimia 50 ya kura.

Lula amekuwa akiandamwa na kashfa za ufisadi na alifungwa jela kwa miezi 18 kabla ya Mahakama ya Juu nchini Brazil kubatilisha hukumu hiyo mwaka jana. Bolsonaro amekuwa akitaja kuwa atayapinga matokeo ikiwa atashindwa huku akidai kuwa Mungu pekee ndie mwenye uwezo wa kumuondoa madarakani na amekuwa akidai bila ya kuwa na ushahidi kwamba mfumo wa kupiga kura wa kielektroniki umezungukwa na udanganyifu.

**DW**

**Da Silva ambaye anatoka kambi ya mrengo wa kushoto, pia aliwahi kuiongoza nchi hiyo kutoka mwaka 2003 hadi 2010.**

# Waliopindua serikali,wapinduliwa Burkina Faso

**OUAGADOUGOU,** Burkina Faso

MAOFISA wa jeshi nchini Burkina Faso, wametangaza kuchukua udhibiti wa nchi katika mapinduzi ya pili mwaka huu wakidai kurejesha amani katika nchi hiyo.

Kupitia taarifa iliyosomwa katika kituo cha televisheni cha serikali, jeshi limetangaza kumuondoa Luteni Kanali Paul-Henri Sandaogo Damiba, ambaye aliingia madarakani kufuatia mapinduzi ya mwezi Januari.

Jeshi linamtuhumu Damiba kushindwa kukomesha uasi wa makundi ya kigaidi.

Kapteni Ibrahim Traore mwenye umri wa miaka 34 ndiye ametangazwa kama kiongozi mpya wa nchi hiyo.

Jeshi pia lilitangaza kufungwa kwa mipaka kuanzia usiku wa manane, pamoja na kusitishwa kwa katiba na kuvunjwa kwa serikali.

Jumuiya ya Kiuchumi ya mataifa ya Afrika Magharibi ECOWAS, imelaani mapinduzi hayo

**DW**

SAFU

MAKALA

# WANAFUNZI SAMIA SCHOLARSHIP WASOMEE UALIMU WA SAYANSI



Na Magabilo Masambu

HIVI karibuni Wizara ya Elimu Sanyansi na Teknolojia kupitia kwa waziri mwenye dhamana, Prof. Adolf Mkenda, ilitangaza ufadhili maalum kwa wanafunzi watakaodahiliwa vyuo vikuu nchini katika mwaka wa masomo 2022/23.

Prof. Mkenda alisema kwa wanafunzi watakaokuwa wamefanya vizuri kidato cha sita katika masomo ya Sayansi, watapata fursa ya kugharamiwa kwa asilimia 100 katika kozi za sayansi watakazozisoma vyuo vikuu, zikiwemo fani za uhandisi, teknolojia, na tiba.

Kwanza, nipongeze wazo lenyewe kwa ujumla wake kwa sababu pengine kumeonekana kuna tatizo la kuwapata wataalam katika fani ambazo wanakwenda kuzisoma kwa ufadhili huo. Panapokuwa na tatizo, watu hukaa chini na kuona ni kwa namna gani wanaweza kulitatua. Sina shaka na wazo lakini tunaweza kutofautiana katika utekelezaji wake.

Sote tutakubaliana kwamba kuna umuhimu mkubwa wa kuhamasisha na kushawishi kwa kila namna vijana wetu wasome masomo ya sayansi kwani dunia ya leo bila sayansi hakuna jambo litafanyika. Kwa hiyo lazima tuwe na wanasayansi wengi zaidi katika fani za sayansi ili kulisaidia taifa katika nyanja hiyo tukizingatia tuko katika ulimwengu wa kidigitali. Pamoja na juhudi hizi za wizara, mtazamo wangu katika hili uko tofauti kidogo. Ikiwa vijana hawa watapata ufadhili na kusoma fani hizo zilizoainishwa, maana yake ni kwamba watakapomaliza wataajiriwa, watajiajiri au wakikosa ajira rasmi wataamua kufanya shughuli ambazo haziendani na fani walizozisomea. Ikiwa itatokea hivyo, maana yake itailazimu serikali kupitia wizara yenye dhamana ya elimu iendelee tena kutoa ufadhili kila mwaka kwakuwa haitakuwa imemaliza tatizo la upungufu wa wataalam hao.

Kwa maoni yangu, kwa sababu ufadhili huu umetolewa kwa vigezo na masharti kuzingatiwa, basi sharti la kwanza kabisa lingekuwa kuwafanya wote watakaokuwa wamepata ufadhili huo kuwa walimu katika masomo hayo ya sayansi. Hii maana yake ni kwamba ukizalisha walimu wengi wa sayansi awamu ya kwanza, ukatoa ufadhili awamu ya pili na pengine ya tatu, baada ya muda mfupi utapata walimu wengi sana wa masomo ya sayansi ambao wakiajiriwa watazalisha vijana wengi sana katika masomo hayo ya sayansi.

Tatizo la sayansi katika nchi hii si kukosa wahandisi au madaktari. Shida kubwa tuliyo nayo ni upungufu mkubwa wa walimu wa masomo hayo, jambo linalosababisha wanafunzi wachache kuyasoma na mwisho wa siku kushindwa kuyafaulu vizuri kwa sababu walimu waliopo kwenye shule sasa hivi wanazidiwa na idadi ya wanafunzi.

Upungufu wa pili katika utekelezaji wa jambo hili ni kwamba ukitangaza leo kuwa unawapa ufadhili wanafunzi waliofanya vizuri katika masomo ya sayansi, maana yake ufadhili huo utabagua kundi moja la wanafunzi wanaotoka kwenye shule za umma ambao wengi wao hawafanyi vizuri hasa shule za kata ambazo miundombinu mpaka walimu ni tatizo kubwa kuwezesha wafaulu vyema masomo hayo.

Badala yake utakwenda kuwapatia ufadhili kundi moja la wanafunzi wengi wanaotoka shule za binafsi ambazo mazingira yao ya ujifunzaji hayana changamoto kubwa na ndiyo wanaofanya vizuri zaidi katika masomo ya sayansi. Sisemi kwamba wanafunzi wanaotoka shule binafsi hawana haki. Wanayo lakini ni muhimu pia ufadhili huo kuliangazia kundi la watu wa chini kutoka shule za umma hasa za kata.

Kufanya kuwe na usawa wa ufadhili huo ilipaswa kwanza kuzalisha walimu wengi wa masomo hayo ya sayansi, ambao ndio wangeajiriwa katika shule za umma na baada ya muda ndipo ungekuja ufadhili katika fani husika wakati tayari kuna usawa wa wanafunzi kutoka shule za binafsi na zile za umma. Lakini kwa hali ilivyo sasa, kuna hatari ya kusomesha kundi moja tu ambalo pia wazazi wao wengi, wanao uwezo wa kuwasomesha elimu ya chuo kikuu.

Kwa mantiki hiyo, nguvu kubwa ingeelekezwa katika kuzalisha walimu wengi zaidi baada ya muda walimu hao wazalishe wanafunzi wengi zaidi ambao sasa ndio wangekuja kusoma uhandisi na fani nyiginezo kwa ajili ya mahitaji ya nchi. Mpango huu ungekuwa wa muda mrefu, lakini ukawa na matokeo makubwa zaidi huko mbele wa kuzalisha wanasayansi wengi.

Kwa kuwa vyuo havijafunguliwa, hatujachelewa, hivyo tunaweza kubadili malengo badala ya kuzalisha wahandisi moja kwa moja, hawa watumike kama mbegu zilizopandwa kwenye udongo wenye rutuba na kumwagiliwa maji kila kukicha ili zikishamea, basi zinazaa mavuno mengi zaidi. Kuwafadhili wakaenda moja kwa moja kwenye fani za kujiajiri na kuajiriwa ni sawa na kula mbegu ukategemea katika msimu wa kilimo utavuna bila kupanda mbegu.

Sambamba na wazo la kuzalisha walimu wengi wa sayansi miundombinu pia ni muhimu kuboreshwa, hasa kwenye shule zetu za kata ili tukishakuwa na mazingira sawa, tutaweza kushindana sawa na wengine, ili ufadhili unapotoka kusiwe na kundi linaloachwa kwa kuwa mazingira na uhaba wa walimu umekuwa sababu.

**0689157789**
**magabilomjalifu@gmail.com**
**ARUSHA-TANZANIA**

BURUDANI ILIYOTIKISA ENZI HIZO

## *Kisa cha mwanamuziki aliyeuawa kwa mapanga sababu ya nyumba ndogo - 1*



Na Adam Fungamwango

"KUOA tunaoa lakini tukumbuke yaliyotendeka kwa George Mukabi. George alipooa bibi akakimbia kwa kumfuata akauawa bure. Wazazi wa Mukabi walipata hasara, kupoteza mali na mtoto wao. Wale ambao hatujaoa kweli ndugu zangu, tukifikiri hilo hatutooa tena."

Haya ni mashairi ya wimbo uitwao 'Kifo cha Mukabi', ambao umetungwa na kuimbwa na mwanamuziki John Mwale kutoka Kenya. Alitunga wimbo huo ulio kwenye mtindo wa 'twist' mwanzoni tu mwa miaka ya 1960, baada ya kifo cha kinyama cha mwanamuziki mwenzake, George Mukabi.

Mukabi alikuwa mwanamuziki maarufu, si nchini Kenya tu alikozaliwa, hata nchini Tanzania alikuwa na mashabiki lukuki kutokana na nyimbo zake kali na kugusa wengi wakati huo.

Kifo chake si tu kwamba kilileta pigo kwa mashabiki wa muziki ukanda wa Afrika Mashariki na Kati bali kilileta taharuki kubwa kutokana na mazingira yenyewe.

Itakumbuka kuwa wakati huo teknolojia haikuwa kubwa sana miaka ya 1950 hadi 1970 na nyimbo hizo zilipatikana kwenye santuri au sahani ambazo zilijulikana kama GV.

Ni miaka ambayo nyimbo za wanamuziki hao zilipigwa na magitaa baridi, yaani yasiyotumia umeme, maarufu kama 'magalatoni' zikihamishwa mapigo ya chupa, ngoma au manyanga, mbao au bati ili kunogesha muziki. Hakukuwa na vyombo vingi.

Pamoja na hayo wanamuziki wa enzi hizo walikuwa mahiri sana kwani pamoja na uduni kwa vyombo, walirekodi nyimbo mbalimbali zilizokuwa kwenye santuri ambazo zilivuma na kupendwa sana ukanda wa Afrika Mashariki na Kati.

Tanzania, wakati huo ikiitwa Tanganyika, mpaka baada ya uhuru na baadaye kuwa Tanzania ilipoungana na Zanzibar mwaka 1964, kulikuwa na wanamuziki waliovuma sana wa aina ya hiyo ya muziki ambao mara nyingi ilikuwa 'twist' benga na nyinginezo kama John Ondolo Chacha aliyevuma na wimbo wa 'Mbuga zetu Tanzania' uliokuwa kiashirio cha kipindi cha 'Mbuga Zetu' kwenye redio ya taifa, maarufu kama Radio Tanzania Dar es Salaam (RTD) na Omari Kungubaya ambaye yeye alitamba na wimbo wa 'Salamu za Wagonjwa' uliokuwa kiashirio cha kipindi cha kilichokuwa na jina hilo hilo.

Congo ya Kibelgiji, sasa Jamhuri ya Kidemokrasi cha Congo, kulikuwa na wanamuziki waliopendwa mno nchini wao na nyimbo zao kama Jean-Bosco Mwenda wa Bayeke, Edward Masengo, Losta Abelo, Uganda mwanamuziki aliyekuwa maarufu Bongo ni Charles Sonko na dada yake Frida Sonko. Nchini Zambia kulikuwa na Nashil Pitchen na Peter Tsosi, huku Kenya kulikuwa na kina Daudi Kabaka, John Zenze, John Mwale, Fadhili William pamoja na Mukabi.

Mkenya huyo alizaliwa 1930 na kuuawa mwaka 1963 akiwa kijana tu wa miaka 33 na tayari alikuwa ameshaanza kupata mafanikio kwenye muziki.

Muziki wake ulivuka mipaka ya Kenya na kuwa na mashabiki wengi Tanzania akitamba na nyimbo kama 'Sengula Nakupenda', 'Kweli Ndugu' na 'Mtoto Si Nguo'.

Kabla ya kuelezea kisa kizima kilichosababisha kukatishwa nyota, hebu tuangalie mashairi ya nyimbo zake tatu ambazo ndizo zilizokuwa zikitamba

"Sengula ninakupenda, si nikuwa napenda, Sengula we kweli Sengula wangu, si nilikuwa nakupenda?

"Ni vizuri tupendane, nyumba ikawa na heshima, Sengula we kweli Sengula wangu si nilikuwa nakupenda. Ninachoka na mambo yako, Sengula we kweli Sengula wangu si nilikuwa nakupenda." Huu ndio wimbo bora zaidi na ulikuwa ukimtambulisha mwanamuziki huo na kumpatia sifa na uliuza nakala nyingi mno.

"Mtoto si nguo utaomba mtu, ukikosa mtu baba, ukikosa wako utalia sana baba. George mwamba sina wangu mie, nakosa wangu ee ninalia sana baba." Nao ulipendwa sana nchini Tanzania na kufuatia ule wa 'Kweli Ndugu"

"Kweli wangu sikilizeni niwambieni, kwa kuoa nilikooa bibi mmoja mrembo, sasa kaleta harasa kuvunjavunja vikombe, kuvunja vunja sahani.

"Na wandugu wangu wote walikataa, walisema afunge aende, hatutaki hasara, avunjavunja vikombe, avunjavunja sahani."

Alitunga na kuimba nyimbo nyingi sana kwa muda mfupi tu wa maisha yake, lakini hizo tatu zilitia fora sana hasa nchini Tanzania.

**Sms - (0716 350534)**

ITAENDELEA JUMAPILI

# HADITHI

# Mwisho wa Mauaji-21

PRINCE Petit ni kijana aliyelelewa kwenye mazingira ya ajabu. Amelelewa na baba yake mzazi tu bila mama. Madada wa kazi waliopewa kazi ya kumlea walipewa mkataba wa mwaka mmoja tu na wanapomaliza hawakuongezwa. Hakupelekwa shule yoyote ile badala yake walimu walilipwa pesa kwa ajili ya kumfundisha nyumbani tu. Hata alipokuwa akipata nafasi ya kwenda kufurahia maisha na kuitazama dunia nje ya nyumba yao, alipewa angalizo la kutozoeana na mtu yeyote yule. Aliingiziwa falsafa na vitu vingine kichwani mwake mpaka akawa na tabia ambazo ni tofauti na umri wake. Akiwa na miaka mitano tu, alianza kufundishwa kulenga shabaha na alipofikia miaka minane alikuwa na uwezo wa kutumia bastola ya aina yoyote ile na angeweza kuajiriwa kwenye shirika lolote la kijasusi duniani. Anapofika umri wa miaka 25, baba yake, Mzee Pokwa anamtuma kazi. Kazi ya kuua na kulipiza kisasi. Ni kwa nini? Anakwenda kumuua nani? Kwa nini baba anayejua mkasa mzima asiende mwenyewe? Kitu gani kilichotokea huko nyuma? Nakala yako ya Nipashe itakufanya kujua kilichopo nyuma ya pazia.

**Na Adam Fungamwango**
(0716 350534)




Mzee Pokwa alidhani kuwa Prince ametoka alipojificha. Ghafla akajichomoa alipojificha kwa lengo la kumchapa risasi Prince. Badala yake akashtukia hakuna mtu, ila ni kitu kimerushwa. Akataka kurudi lakini akawa amechelewa.

"Simama hivyo hivyo, ukirudi nyuma robo hatua tu, natawanya ubongo." Ilikuwa ni sauti ya Prince ikimwamrisha mzee Pokwa, lakini papo hapo ikiambatana na sauti ya risasi ambayo aliipiga sawia kwenda kupiga mkono wake wa kulia uliokuwa umeshika bastola. Pamoja na mkono wake kuvuja damu na kuonekana una majeraha yaliyoambatana na maumivu makali, mzee Pokwa bado hakukubali kirahisi.

"Hivi unadhani ndiyo utafanikiwa? Nimekwambia huwezi kuniua kirahisi, weka bastola yako chini usalimu ari, angalau naweza kukusamehe." Akasema kwa sauti ya kijeuri, hasira, kujiamini, lakini akionekana kuwa na maumivu.

Hilo pekee lilimfahamisha kuwa bado mzee Pokwa kuna kitu anategemea. Kwa hali ya kawaida angeweza kunyoosha mikono juu. Kengele ya hatari ikagonga kwenye kichwa cha Prince kuwa inawezekana ikawa bado yuko hatarini.

Alisogea nyuma kwa tahadhari ili yoyote atakayeingia awe na tahadhari. "Unasikia mzee, baada ya kusikia historia nzima ya kweli kuhusu wazazi wangu na ulichowafanyia, niliapa kulipiza kisasi. Yeyote aliyewaua au kusababisha vifo vyao, nitamuua mimi mwenyewe kwa mkono wangu. Ulinipa historia ya uongo na kuwaua watu waliokuwa wanisaidie, ukajifanya wewe ni baba yangu. Kosa ulilolifanya ni kuniacha hadi nimekua, ungeniua pale pale wakati niko mdogo, leo ndiyo utajutia ulichokifanya, kwa heri mwanahizaya mkubwa wee..."

Kauli hiyo ilimalizika kwa sauti mbili za risasi zilizotawanya ubongo wa mzee Pokwa. Alinguka chini kama mzigo. Akalala kwenye dimbwi la damu lililochanganyika na ubongo. Ilikuwa taswira ya kutisha na kusikitika kwa wakati mmoja.

"Mikono juu." Sauti nyingine kutoka kusikojulikana iliunguruma. Prince hakuwa na ujanja, aliangusha bastola yake chini na kunyoosha mikono juu. Alijua ndio mwisho wake. Ghafla watu wawili walimfuata pale na kuanza kumsachi. Nyuma yao ndiko alikokuwa yule ambaye alikuwa na bastola.

**"Wewe ndiye uliyepiga simu?" Askari mmoja akamuuliza Prince.**

Baada ya kuhakikisha kuwa hana kitu chochote ambacho kingekuwa na madhara, waliiokota bastola aliyokuwa ameiangusha.

Ndipo alipogundua kuwa wale walikuwa maaskari na si watu wa mzee Pokwa kwa sababu alipoongozwa mbele na kutokea uani aliwakuta askari kanzu wengine ambao waliwaweka chini ya ulinzi watu wanne.

"Ulichokosea wewe umeua, kwa nini umemuua yule mzee? Alitakiwa kwenda kujibu mashtaka yanayomkabili. Prince hakujibu kitu mdomoni. Lakini moyoni alijibu "Niliapa kuwa nitamuua mwenyewe kwa mkono wangu, tangu

siku ile nilipoamshwa kwenye usingizi wa pono na mama yangu mdogo Hidaya."

Alitegemea kuwaona askari pale muda ule, ila hakujua kuwa mzee Pokwa pia alikuwa na watu wake ambao walikuwa wametanda kwenye nyumba ile bila yeye kujua.

Ni yeye mwenyewe ndiye aliyewapigia simu alipotoka kwa kina Hidaya. Alipotoka huko hakuwa na uhakika kama anakokwenda kutakuwa salama. Alijua kabisa mzee Pokwa hakuwa mtu wa mchezo mchezo, inawezekana akajua mchezo mzima kuwa hakumuua mama huyo, hivyo kummaliza yeye.

Angejua kuwa kama Hidaya hakuuawa, ina maana atakuwa amemhadithia kila kitu. Ndiyo maana alipotoka huko, kabla hajaenda nyumbani kwao, aliwapigia simu askari polisi wa kituo cha Oysterbay na kuwaeleza kuhusu habari yote kuhusu mzee Pokwa, pamoja na sehemu wanayoishi ambayo ni Kinondoni Moscow.

Hata hivyo, alichofanya ni kuwadanganya kuhusu muda wa kufika ili atekeleze kile alichopanga ambacho ni kumuua Pokwa kwa mkono wake mwenyewe.

Angewaeleza muda sahihi, wangefika kabla ya kutekeleza alichokikusudia. Alichokifikiria ndicho alichokiona. Tayari mzee Pokwa alikuwa na wasiwasi na kijana wake kuhusu mwenendo wake. Pia kwa sababu alikuwa amemaliza wote aliowahitaji kama alivyodhani, hakutaka Prince aendelee kuishi.

Kuendelea kuishi naye ni sawa na kuishi na joka kubwa ndani linaloweza kukudhuru muda wowote. Kwa hiyo alileta vijana watano wa kazi. Shughuli yao ilikuwa kukabiliana na Prince. Pokwa hakujidanganya kuwa Prince si mtu hatari kwa sababu alimtengeneza mwenyewe.

Watu wanne walijificha nje ili kukabiliana na chochote kinakachotokea na mmoja alijificha ndani. Kwa bahati mbaya malengo yalifanana kwa siku moja. Kila mmoja alitaka kumuua mwenzake siku hiyo. Prince alikuwa mjanja kwa kumuua mmoja wa watu hao na mwenyewe Pokwa. Alikuwa pia ameshawataarifu polisi, vinginevyo naye angeuawa na wale waliokuwa nje waliowekwa kama akiba.

Askari polisi walipofika kwanza kabisa walianza kuwakamata kirahisi wale wa nje ambao akili yao ilikuwa wanasikilizia yanayotendeka ndani ili wakatoe msaada ukihitajika. Walipoingia ndipo walipomkuta Prince aliyewaarifu kufika pale saa mbili usiku, akimmalizia mzee Pokwa na yeye wakamdaka.

"Wewe ndiye uliyepiga simu?" Askari mmoja akamuuliza Prince.

"Ndiyo."

"Sasa ndugu yangu, unatuita, halafu na wewe unaua?"

"Nisingeua, ningeuawa,"akajibu.

Kitu ambacho Polisi walichogundua ni kwamba watu wale ndio wanahusiana na kesi za kuuawa kwa Sabri, Nassor Hassan na Hussein.

*Itaendelea Jumapili*




# KITUO CHA KUTIBU NGOZI, NYWELE CHAZINDULIWA DAR

SUALA la urembo unaotokana na vipodozi vya asili unazidi kupigiwa chapuo kutokana na kuwa na faida nyingi kuliko madhara.

Idadi kubwa ya wanawake na wanaume wamegeukia vipodozi vya asili kama njia salama ya kuboresha afya ya ngozi na nywele.

Jana kulikuwa na tukio la kipekee la kuzinduliwa kituo cha QM Beauty ambacho kitakuwa na kazi ya kuhudumia watu kuboresha na kutibu ngozi na nywele kwa kutumia bidhaa zilizotengenezwa kwa vyakula na matunda.

Akizungumza katika uzinduzi huo, Saida Bandawe ambaye ni mkurugenzi wa kampuni ya QM Beauty, amesema kituo hicho ni mbadala wa watu wanaohitaji ngozi na nywele kuwa salama wakati wote.

Bandawe amesema wazo la kufungua kituo hicho na kutengeneza vipodozi asili alilipata baada ya kusumbuliwa na matatizo ya ngozi muda mrefu kutokana na matumizi ya vipodizi vya viwandani.

"Niliwaza kitu gani kinaweza kuwaokoa watu wengi walioathirika na matumizi ya bidhaa zenye sumu, hapo ndipo nikaanza kubuni bidhaa zangu kwa kutumia matunda na vyakula na kuleta matokeo mazuri kwa kila anayetumia," alisema Bandawe.

Amesema kutokana na ubunifu wake huo, ameajiri watu wa kumsaidia katika kituo chake kilichoko karibu na ubalozi wa Kenya jijini Dar es Salaam.

"Bidhaa za vipodozi ninavyotengeneza vinasifika kwa usalama kiafya na ndio maana nimeona ni vyema kuwanusuru wengine ngozi na nywele zao kwa kuja hapa kupata huduma na ushauri," ameongeza.

Mgeni rasmi ambaye ni Mwenyekiti wa Misa Tan, Salome Kitomari, alimpongeza Saida kwa kuwa na maono ambayo kwa sasa licha ya kusaidia watu, pia imeongeza ajira kwa vijana.

Amesema matumizi ya vipodozi vinavyotokana na bidhaa asili ni salama na kuwataka watu kumuunga mkono mjasiriamali huyo kwa kutumia kwa wingi.

"QM Beauty imekuja wakati muafaka kwani itasaidia watu kuepuka matumizi ya vipodozi vyenye sumu na kuathiri ngozi na nywele zao, nawaomba watu kuchangamkia fusra hii kwa kutumia kwa ajili ya afya zao na pia kuwainua kiuchumi kwa kibiashara," amesema Kitomari.

# Basata kurudisha maonyesho ya jukwaani

**Na Halfani Chusi**

SERIKALI imesema ipo njiani kurejesha sanaa ya maonyesho ya jukwaani ili kuwawezesha wasanii kujikwamua kiuchumi.

Hayo yalisemwa jana Dar es Salaam, na Katibu Mtendaji Baraza la Sanaa Taifa, Dk Kedmon Mapana, wakati alipohudhuria jukwaa la maonyesho lililoandaliwa na mtandao wa wasanii wanawake Tanzania.

"Salamu zangu ndogo ni kwamba kazi ndio imeanza kwenye sanaa za maonyesho lazima shirikikisho la sanaa za maonyesho kwa namna moja ama nyingine tutafute jambo la kuitikisa nchi.

Kwa hiyo mfuko wa sanaa na utamaduni unaoanzishwa wito wangu kwa wasanii hakikisha unafanya kazi ukiwa umewasilishwa, huku tutahitaji chama cha sanaa unachotoka ili watu wasije wakatumia mwanya huu kujipatia mkopo bila kujulikana wanakotokea

Mwenyekiti Kutoka Mtandao wa Wasanii Wanawake Tanzania, Agnes Lukanga, alisema onyesho hilo lilikuwa mahususi kwa kutoa mrejesho wa mafunzo yaliyofanywa na mradi wa "tuseme tusichoke" ambao ulijikita zaidi kuangalia namna wasanii wanawake walivyoathirika kipindi cha corona na namna ya kuwasaidia

"Baada ya hapo tulikuwa na mafunzo mengine kwa wasanii wenyewe katika kuwahoji walisema waliathirika na mambo mengi ikiwamo ukatili wa kingono, ukatili wa kijinsia, na katika hilo tulibaini kipindi hicho wasanii walipata shida na wengine walishindwa kuendelea na kazi ya sanaa.

# HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### MBAPPE ALIMTAJA RASHFORD

KYLIAN Mbappe aliipatia PSG orodha ya wachezaji wanne aliokuwa anawataka msimu huu wa joto ikiwa ni pamoja na mshambuliaji wa Manchester United na Timu ya Taifa ya England, Marcus Rashford (24). ***(RMC Sport)***

### NKUNKU SAFI CHELSEA

MSHAMBULIAJI wa RB Leipzig, Christopher Nkunku mwenye umri wa miaka 24 tayari amekamilisha uchunguzi wa kimatibabu kabla ya kujiunga na Chelsea kwa ada ya pauni milioni 52 katika dirisha lijalo la usajili. ***(Bild)***

### HAALAND ALIITAKA CHELSEA

MSHAMBULIAJI wa Manchester City na Timu ya Taifa ya Norway, Erling Haaland mwenye umri wa miaka 22, alifikiria kuhamia Liverpool katika dirisha la usajili la majira ya joto, lakini hakufikiria kutua Manchester United. ***(Star)***

### POCHETTINO ATAJWA VILLA

KLABU ya Aston Villa inamchunguza kocha wa zamani wa Paris St-Germain, Mauricio Pochettino na kocha wa Villarreal, Unai Emery huku kukiwa na uvumi juu ya mustakabali wa Steven Gerrard. ***(Football Insider)***

### JESUS ALITAKA UHURU

MSHAMBULIAJI wa Arsenal na Brazil, Gabriel Jesus amesema alihitaji mabadiliko kutoka kwenye mfumo wa Pep Guardiola katika klabu ya Manchester City na sasa anajisikia "huru" kucheza chini ya Mikel Arteta. ***(ESPN)***

### MADDISON AITAMANI SPURS

TOTTENHAM Hotspur inamfuatilia kwa karibu, James Maddison wa Leicester City, huku kiungo huyo wa kati wa England mwenye umri wa miaka 25 "anataka sana" kuhamia klabu hiyo ya Kaskazini mwa London. ***(Football Insider)***

### PILISIC KUPATA NAFASI

KOCHA wa Chelsea, Graham Potter yuko tayari kumpa winga wa Marekani, Christian Pulisic mwenye umri wa miaka 24 nafasi ya kujidhihirisha Stamford Bridge kabla ya kufanya uamuzi kuhusu mustakabali wake. ***(90min)***

### POTTER, LUKAKU KUTETA

KOCHA Graham Potter hajafunga mlango kwa mshambuliaji wa Ubelgiji, Romelu Lukaku kurejea Chelsea baada ya muda wake wa mkopo na Inter Milan na anatarajiwa kufanya mazungumzo na mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 29 mwishoni mwa msimu huu. ***(ESPN)***

### PSG YAFUNGUKA ILIPOKOSEA

MKURUGENZI wa michezo wa Paris St-Germain, Luis Campos amesema klabu hiyo ilifanya makosa kwa kuwasajili fowadi wa Brazil Neymar mwenye umri wa miaka 30 na mshambuliaji wa Ufaransa, Kylian Mbappe (23). ***(Mail)***

### LUIZ KUONDOKA VILLA

KOCHA wa Aston Villa, Steven Gerrard amesema Douglas Luiz mwenye umri wa miaka 24, hajakaribia kusaini mkataba mpya na klabu hiyo, na hivyo kuongeza nafasi ya Arsenal kumsajili kiungo huyo wa kati wa Brazil. ***(Sun)***

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA



# PSG : USAJILI WA NEYMAR, MBAPPE HAUKUWA SAHIHI

Bosi wa ufundi amekiri klabu hiyo ilikosea kuwanasa mastaa hao...

**PARIS, Ufaransa**

MKURUGENZI wa Michezo wa Paris Saint-Germain, Luis Campos, amekiri walifanya makosa kwa kuwasajili Neymar na Kylian Mbappe katika klabu hiyo.

Nyufa zimeonekana kwenye uhusiano kati ya mastaa hao wawili huku Neymar wiki iliyopita akitoka nje ya mahojiano alipoulizwa kuhusu mchezaji mwenzake alipokuwa katika majukumu ya kimataifa na Brazil.

Mabingwa hao wa Ligue 1 wamewekeza fedha nyingi kwa wawili hao, huku Neymar akigharimu ada ya rekodi ya dunia ya pauni milioni 190 mwaka 2017, ikifuatiwa na Mbappe ambaye awali kwa mkataba wa mkopo kabla ya uhamisho wake wa kudumu wa pauni milioni 159 kutoka Monaco.

Akizungumza na jarida la France Football, Campos alikiri kusajili wachezaji wote wawili huenda haukuwa uamuzi wa busara wa klabu.

"Tulifanya makosa siku za nyuma kusajili wachezaji wawili katika nafasi moja. Dirisha la uhamisho sio zuri kwa sababu tunakosa wachezaji kwenye nafasi muhimu na kwa sababu tuna mwingiliano wa wachezaji katika nafasi nyingine," alisema.

Ingawa matokeo ya Neymar na Mbappe bado hayajaweza kuiletea klabu hiyo ushindi mnono wa Ligi ya Mabingwa karibu zaidi wamekaribia kushinda kombe hilo ni kushindwa kwao na Bayern Munich katika fainali ya 2020, wote wamefanikiwa ndani ya nchi.

Mbrazil huyo amefunga mabao 111 katika michezo 155 akiwa na kikosi hicho cha kocha, Christophe Galtier na kushinda mataji manne ya ligi.

Mbappe amekuwa na kiwango sawa, akiwa amefunga mabao 181 katika mechi 226 akiwa Parc de Princes, pamoja na mataji manne ya ligi.

SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!

CHEZA USHINDE JACKPOT TZS. 360,

MECHI KALI

MANCHESTER CITY

VERSUS

MANCHESTER UTD

1 | 1.38

X | 4.83

2 | 6.69

PIGA *150*87#

Karibu SportPesa
1. Bet Sasa
2. Michezo zaidi
3. JACKPOT
4. Weka Pesa
5. Akaunti yangu
6. Toa Pesa
7. Matokeo ya Bet/Mechi
00. Toka


SportPesa

SPORTPESA.CO.TZ

HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, TUPIGIE:
0764115588, 0677115588
0685115588 GBT:0249
18+

@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# MAGUIRE NJE UNITED IKIWAKABILI MAN CITY




**MANCHESTER, England**

HARRY Maguire hataichezea Manchester United katika mechi dhidi ya Manchester City kutokana na jeraha, lakini Erik ten Hag ana imani anaweza kuwa katika kiwango chake bora atakaporejea.

Nahodha huyo wa United amevumilia msimu mgumu, akipoteza nafasi yake katika ngazi ya klabu na kisha kufanya vibaya kwa England licha ya kuungwa mkono na Gareth Southgate, huku makosa yake yakichangia Ujerumani kuongoza kwa mabao 2-0 katika sare ya magoli 3-3 kwenye mechi ya Ligi ya Mataifa ya Uefa iliyochezwa Jumatatu iliyopita.

Kumekuwa na wito wa kutaka Maguire aachwe na Southgate, lakini kwanza anakabiliwa na kibarua kigumu kuwapita Raphael Varane na Lisandro Martinez kurejea kwenye kikosi cha Ten Hag cha United.

Hilo halitafanyika katika mchezo wa dabi ya Jumapili, kwani Ten Hag alifichua beki huyo wa kati ndiye pekee aliyekuwa na jeraha, ambaye anatarajiwa kukosa mchezo huku Anthony Martial na mchezaji bora wa mwezi wa Ligi Kuu England, Marcus Rashford wakirejea.

Hata hivyo, kocha huyo wa United aliulizwa anachoweza kufanya ili kumsaidia Maguire kurejea katika ubora wake.

"Kwanza kabisa, sina budi kumfundisha," alisema Ten Hag. "Lazima nimuunge mkono, lakini namuunga mkono kwa sababu ninamwamini, kipindi ambacho nilikuwa nikifanya naye kazi katika maandalizi ya msimu uliopita, alikuwa mzuri, naweza kusema ni mzuri sana.

"Unaona kazi yake: ana takribani mechi 50 za England, tayari akiwa na Leicester na United amefanya vizuri sana. Unachokiona ni uwezo wa juu."

# Madrid kumwongeza mkataba Millitao

**MADRID, Hispania**

REAL Madrid ya Hispania imepanga kumwongezea mkataba beki wake kitasa, Eder Millitao raia wa Brazil baada ya kuwa na wakati mzuri klabuni hapo.

Beki huyo aliejiunga na Real Madrid mwaka 2019 akitokea FC Porto ya Ureno alicheza kwa msimu mmoja kwa ubora na mabingwa hao wa Ulaya kuvutiwa naye na kumsajili.

Millitao hakuwa na msimu mzuri ndani ya Real Madrid katika misimu miwili ya kwanza pamoja na kutokupata nafasi kwa sababu ya mabeki waliokuwapo klabuni hapo wakiwamo Raphael Varane na Sergio Ramos ambapo walisababisha ufinyu wa nafasi lakini baada ya kuondoka beki huyo alianza kupata nafasi na akawa na msimu bora sana mwaka 2021/22.

Mabingwa hao wa Ulaya wana mpango kumwongezea mkataba mchezaji huyo ambao utamfanya abakie hapo hadi mwaka 2028 na wanatarajiwa kuweka kipengele kigumu cha kumuuza.

Millitao amekua miongoni mwa wachezaji muhimu ndani ya kikosi cha Carlo Anchelotti tangu kocha huyo atue klabuni hapo.



,499,520

# AZAM YALIA NA WAAMUZI IKIKUBALI KICHAPO MBEYA

**Na Adam Fungamwango**

IKIFUNGWA kwa mara ya kwanza katika msimu huu kwenye Uwanja wa CCM Sokoine jijini Mbeya dhidi ya Prisons hapo juzi, Azam FC imesema haikupoteza mechi hiyo kwa sababu haikuwa bora, ila ilitokana na mwamuzi kutokuwa bora.

Ofisa Habari wa Azam FC, Thabit Zakaria, alisema kuna vitu ambavyo havikuwa ndani ya uwezo wa timu yao pamoja na Prisons vilivyowanyima ushindi na kutaja wazi kuwa ni mwamuzi wa kati, Hans Mabena pamoja na wasaidizi wake ambao walichezesha mechi hiyo.

Zakaria alisema waamuzi 'waliinyonga' timu yao na kusababisha kukosa ushindi katika mechi hiyo iliyomalizika kwa Prisons kushinda bao 1-0.

"Kupoteza mchezo katika mazingira kama yale ni tatizo zaidi, unalazimishwa upoteza, ina maana kuna watu walikubaliana lazima timu hii ifungwe, ipoteze mchezo, inauma sana," alisema Zakaria maarufu Zaka Zakazi.

Pamoja na hayo aliwapongeza Prisons kwa ushindi na kusema walicheza vizuri, lakini anaamini wao walicheza vizuri zaidi.

"Waamuzi walitukatili katika maeneo ambayo yalikuwa muhimu kupata mabao na ushindi. Mshambuliaji wetu Kipre Junior ndani ya dakika 10 za kwanza alishikwa mkono na Michael Ismail wa Prisons akaanguka, lakini hakuna maamuzi yaliyotokea, mwamuzi kama angekuwa upande wetu tulistahili kupata penalti.

Kipindi cha pili Jumanne El Fadhili aliushika mpira, mwamuzi hakuchukua hatua. Sisi hatukufungwa kwa sababu hatukuwa bora, ila tumepoteza kwa sababu waamuzi hawakuwa bora," alilalamika kiongozi huyo.

Bao pekee katika mechi hiyo lilifungwa na Jeremiah Juma, sekunde chache tu baada ya mapumziko na kuifanya Prisons kupata ushindi wa pili katika Ligi Kuu Tanzania Bara msimu huu huku Azam ikipoteza kwa mara ya kwanza baada ya kucheza mechi nne.

Hata hivyo msimu huu Azam imekuwa na rekodi nzuri kwani msimu uliopita ilipoteza kwenye mechi ya pili tu ya Ligi Kuu, ilipofungwa mabao 2-1 na Polisi Tanzania baada ya kutoka sare ya goli 1-1 kwenye mechi ya ufunguzi dhidi ya Coastal Union.



Wachezaji wa Timu ya Soka ya Taifa ya Wasichana wa umri chini ya miaka 17 (Serengeti Girls), wakifanya mazoezi kwenye Uwanja wa Portsmouth, England kwa ajili ya kujiandaa na fainali za Kombe la Dunia zitakazofanyika kuanzia Oktoba 11 hadi 30, mwaka huu nchini India. **PICHA: TFF**

## Yanga, Al Hilal

INATOKA UK. 24

Naye Kocha Msaidizi wa Yanga, Cedric Kaze, amesema kuifikiria zaidi mechi dhidi ya Al Hilal yanaweza kusababisha wakafanya vibaya katika mechi ya Ligi Kuu dhidi ya Ruvu Shooting itakayochezwa kesho.

Kaze alisema sasa hivi kila mtu anaizungumzia zaidi mechi dhidi ya Al Hilal na kwao wanauona huo ni mtego na endapo wataweka akili katika mchezo huo wanaweza kupoteza mechi dhidi ya Ruvu Shooting na hawataki hilo litokee.

## Simba, Dodoma Jiji majaribuni

INATOKA UK. 24

kimejiandaa kulingana na ukubwa wa mpinzani wanayekutana naye lakini wakiamini timu yao pia inaundwa na wachezaji wenye uzoefu na utulivu.

Kibacha alisema wanafahamu Simba ina wachezaji wazuri lakini wao wamejipanga kuwaonyesha ubora walionao na hatimaye watahakikisha wanapata matokeo mazuri katika mchezo huo.

"Tunatambua Simba ni timu kubwa na bora, tutaingia kwa tahadhari kubwa na tunawaheshimu, kwa kufuata maelekezo ya benchi la ufundi kwa kuzingatia madhaifu yao tutapata matokeo chanya na kuwapa ushindani mkubwa," alisema Kibacha.

Mechi nyingine ya ligi hiyo itakayochezwa leo itakuwa ni kati ya wenyeji wa Manungu Complex, Mtibwa Sugar ya Turiani, Morogoro dhidi ya Mbeya City kutoka jijini, Mbeya.

Ligi hiyo itaendelea tena kesho kwa vinara, Yanga kuwakaribisha Ruvu Shooting kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, timu zote zikiwa na kumbukumbu ya ushindi katika michezo yake iliyopita.


# JACKPOT
## MECHI WIKI HII

BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE 13

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 04/10/22 | 19:45 | Marseille vs Sporting Lisbon | 2.23 | 3.40 | 3.15 |
| 02. 04/10/22 | 21:45 | Plymouth vs Sheffield Wed | 2.56 | 3.26 | 2.61 |
| 03. 04/10/22 | 21:45 | Hartlepool vs Doncaster | 2.65 | 3.20 | 2.55 |
| 04. 04/10/22 | 21:45 | Walsall vs Northampton | 2.54 | 3.19 | 2.69 |
| 05. 04/10/22 | 22:00 | Porto vs Bayer Leverkusen | 2.20 | 3.49 | 3.14 |
| 06. 04/10/22 | 22:00 | Ajax vs Napoli | 2.20 | 3.69 | 2.99 |
| 07. 04/10/22 | 22:00 | Cardiff vs Blackburn | 2.48 | 3.19 | 2.74 |
| 08. 05/10/22 | 21:45 | Hull City vs Wigan | 2.45 | 3.19 | 2.79 |
| 09. 05/10/22 | 21:45 | Rotherham vs Millwall | 2.41 | 3.19 | 2.85 |
| 10. 05/10/22 | 22:00 | Sevilla FC vs Borussia Dortmund | 2.80 | 3.40 | 2.34 |
| 11. 05/10/22 | 22:00 | Preston vs West Bromwich | 2.86 | 3.21 | 2.39 |
| 12. 06/10/22 | 19:45 | Pyunik Yerevan vs Zalgiris | 2.40 | 3.22 | 2.92 |
| 13. 06/10/22 | 22:00 | Midtjylland vs Feyenoord | 2.89 | 3.64 | 2.23 |

## MECHI ZA USHINDI

"1" - NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA
"X" - NI TIMU KUTOKA SARE
"2" - NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

## JUMAPILI - 02/10/2022

| MUDA | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 13:30 | 3316 | Lazio vs Spezia | 1.39 | 4.70 | 6.79 |
| 14:00 | 4771 | Lorient vs Lille | 2.76 | 3.51 | 2.34 |
| 14:00 | 5834 | Stoke City vs Watford | 2.37 | 3.15 | 2.95 |
| 15:00 | 1094 | Silkeborg vs Horsens | 1.71 | 3.67 | 4.62 |
| 15:00 | 1930 | Midtjylland vs Viborg FF | 1.67 | 3.76 | 4.71 |
| 15:00 | 2071 | Espanyol vs Valencia | 2.64 | 3.20 | 2.64 |
| 15:00 | 2268 | Asteras Tripolis vs OFI Crete | 1.86 | 3.32 | 4.23 |
| 15:15 | 1255 | FC Sion vs FC Winterthur | 1.77 | 3.83 | 4.04 |
| 15:30 | 1318 | SBV Excelsior vs Utrecht | 4.40 | 4.10 | 1.64 |
| 15:30 | 4599 | Josko Ried vs SCR Altach | 1.95 | 3.34 | 3.49 |
| 15:30 | 4861 | TSV Hartberg vs Austria Klagenfurt | 2.85 | 3.39 | 2.20 |
| 16:00 | 1178 | AC Ajaccio vs Clermont Foot | 2.20 | 3.06 | 3.41 |
| 16:00 | 1524 | Toulouse vs Montpellier | 1.95 | 3.61 | 3.51 |
| 16:00 | 1833 | Varbergs Bois vs BK Hacken | 3.49 | 3.54 | 1.89 |
| 16:00 | 1896 | Sampdoria vs Monza | 2.23 | 3.30 | 3.05 |
| 16:00 | 2024 | Lecce vs Cremonese | 2.06 | 3.31 | 3.41 |
| 16:00 | 2667 | Olympiakos vs Atromitos | 1.30 | 4.84 | 10.08 |
| 16:00 | 3807 | Sassuolo vs Salernitana | 1.98 | 3.64 | 3.34 |
| 16:00 | 3953 | Manchester City vs Manchester Utd | 1.38 | 4.83 | 6.69 |
| 16:00 | 4350 | Troyes vs Reims | 2.45 | 3.27 | 2.77 |
| 16:00 | 5237 | AJ Auxerre vs Brest | 2.61 | 3.31 | 2.56 |
| 16:30 | 3475 | Zenit St Petersburg vs Rostov | 1.28 | 5.39 | 8.98 |
| 16:30 | 4482 | Hertha BSC vs Hoffenheim | 2.69 | 3.54 | 2.34 |
| 17:00 | 2731 | Brondby vs Lyngby | 1.68 | 3.72 | 4.73 |
| 17:00 | 2898 | KAA Gent vs Cercle Brugge | 1.61 | 3.88 | 5.05 |
| 17:00 | 4287 | Konyaspor vs Umraniyespor | 1.62 | 3.77 | 5.22 |
| 17:15 | 3771 | Celta Vigo vs Betis | 2.44 | 3.27 | 2.82 |
| 17:30 | 2114 | Rio Ave vs Santa Clara | 2.40 | 3.11 | 2.96 |
| 17:30 | 2322 | FC Lugano vs Servette Geneva | 2.39 | 3.47 | 2.71 |
| 17:30 | 4640 | FC Luzern vs BSC Young Boys | 3.42 | 3.72 | 1.95 |
| 17:45 | 4371 | Waalwick vs Sparta Rotterdam | 2.17 | 3.31 | 3.16 |
| 18:00 | 2887 | Austria Vienna vs Sturm Graz | 2.51 | 3.30 | 2.51 |
| 18:05 | 5197 | Monaco vs Nantes | 1.53 | 4.22 | 5.43 |
| 18:30 | 2919 | Leeds vs Aston Villa | 2.32 | 3.35 | 2.85 |
| 18:30 | 3202 | Schalke 04 vs Augsburg | 1.94 | 3.54 | 3.54 |
| 19:00 | 2724 | Copenhagen vs Aarhus | 1.74 | 3.57 | 4.53 |
| 19:00 | 3851 | Akhmat Grozny vs Dinamo Moscow | 2.56 | 3.36 | 2.56 |
| 19:00 | 4369 | Atalanta vs Fiorentina | 1.93 | 3.44 | 3.69 |
| 19:30 | 1543 | Kortrijk vs Royal Antwerp | 4.22 | 3.67 | 1.77 |
| 19:30 | 1913 | Volos vs Aris Salonica | 3.42 | 3.27 | 2.09 |
| 19:30 | 5733 | Girona vs Real Sociedad | 3.14 | 3.14 | 2.31 |
| 20:00 | 3156 | Besiktas vs Fenerbahce | 2.37 | 3.52 | 2.71 |
| 20:00 | 3230 | Pacos Ferreira vs FC Arouca | 2.25 | 3.17 | 3.17 |
| 21:00 | 4574 | Emmen vs Heerenveen | 2.85 | 3.21 | 2.39 |
| 21:30 | 1810 | PAOK vs Panathinaikos | 2.50 | 3.07 | 2.87 |
| 21:45 | 4522 | Lens vs Lyon | 2.48 | 3.56 | 2.55 |
| 21:45 | 4692 | Juventus vs Bologna | 1.56 | 3.89 | 5.50 |
| 22:00 | 4375 | Real Madrid vs Osasuna | 1.31 | 5.25 | 8.48 |
| 22:00 | 5869 | St Truiden vs Eupen | 1.76 | 3.62 | 4.33 |
| 22:30 | 3367 | Famalicao vs Boavista | 2.23 | 3.12 | 3.27 |

CHEZA KWA WAJIBU | KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

# Michezo


Jumapili Oktoba 2, 2022

Nipashe




## PSG : Usajili wa Neymar, Mbappe haukuwa sahihi

UKURASA 21




Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa (kushoto), amefanikisha kupatikana kwa Sh. milioni 600 kupitia mashindano ya NMB marathon ambazo zitatumika kwa ajili ya matibabu ya wanawake wenye matatizo ya Fistula hapa Tanzania. Kauli mbiu za mbio hizo ilikuwa ni Mwendo wa Upendo. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# SIMBA, DODOMA JIJI MAJARIBUNI LIGI KUU

## ●●●Mnyama aahidi ushindi ili kujiweka sawa kuelekea mechi ya CAF ambayo...

**Na Saada Akida**

KAZI imerejea, kikosi cha Simba kikiwa bila ya nyota wake kutoka Senegal, Pape Sakho kinatarajia kuikaribisha Dodoma Jiji FC katika mechi ya raundi ya tano ya Ligi Kuu Tanzania Bara itakayochezwa leo kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.

Hata hivyo Simba ambayo imerejea kutoka Zanzibar ilipokwenda kuweka kambi ya muda pia itawakosa nyota wake wengine ambao ni Peter Banda aliyeumia wakati wakicheza mchezo wa kirafiki dhidi ya Malindi na Shomari Kapombe, aliyechanika nyama za paja.

Akizungumza na gazeti hili jijini jana, Kocha Msaidizi wa Simba, Selemani Matola, alisema kuelekea mechi hiyo wamejiandaa vizuri na kikosi chao kipo tayari kupambana ili kuondoka na pointi tatu muhimu dhidi ya timu hiyo kutoka Dodoma.

Matola alisema baada ya kumaliza ziara ya Zanzibar kwa kucheza mechi mbili za kirafiki, sasa wako imara na tayari kuwapa furaha mashabiki wao kwa kuondoka na ushindi katika mchezo huo.

"Mechi yetu dhidi ya Dodoma Jiji FC, sio rahisi kwa sababu msimu uliopita walitusumbua, hatutaingia kwa kuridhika na ukubwa wetu bali wachezaji watatakiwa kusaka ushindi ili tuendelee kujiimarisha katika msimamo wa ligi," alisema Matola.

Kiungo na nahodha huyo wa zamani wa Simba, alisema wanahitaji kupata ushindi katika mechi hiyo ili kuongeza ari ya kikosi kuelekea mchezo wao wa kimataifa dhidi ya De Agosto ambao utachezwa ugenini nchini Libya.

Nahodha Msaidizi wa Simba, Mohammed Hussein (Zimbwe Jr), alisema makocha wamemaliza majukumu yao na sasa kazi kubwa imebaki kwa wachezaji ambayo ni kutafuta pointi muhimu kwa ajili kuendelea kupata matokeo bora.

"Tumejipanga vizuri kuhakikisha tunaondoka na alama tatu, makocha wamemaliza kazi zao kikubwa imebakia kwetu, tumefanya maandalizi mazuri na mechi ya Zanzibar zimetengeneza utimamu wa mwili, tuko tayari kwa ajili ya kusaka ushindi," alisema Zimbwe Jr.

Naye Kocha Msaidizi wa Dodoma Jiji FC, Mohammed Muya, alisema timu yake ilianza vibaya msimu kwa sababu ya kutokuwa na muunganiko ambao kwa sasa umepatikana na wanajiimarisha kuhakikisha wanapata matokeo mazuri dhidi ya Simba.

Muya alisema ushindi waliopata dhidi ya Geita Gold FC siku chache zilizopita umewaongezea hamasa wachezaji wao na wanaamini wataingia kuwakabili Simba kwa kuonyesha kiwango kizuri.

Alisema wamejipanga kuonyesha ushindani mkubwa dhidi ya Simba huku wakiahidi kuwa makini wakati wote wa mchezo.

"Tumefanikiwa kuangalia mechi za Simba zote ikiwamo za kirafiki walizocheza Zanzibar na kuona madhaifu yao, tutahakikisha tunayatumia makosa hayo ili kupata matokeo mazuri na kujiimarisha kwenye msimamo wa ligi," alisema Muya.

Mbwana Kibacha, Nahodha wa Dodoma Jiji FC, aliliambia gazeti hili kikosi chao

INAENDELEA UK . 23

## Yanga, Al Hilal hesabu zakolea

**Adam Fungamwango na Saada Akida**

WAKATI Yanga ikiichukulia Al Hilal ni timu ya kawaida, Kocha Mkuu wa kikosi hicho chenye makao yake Khartoum, Sudan, Florent Ibenge, ameandaa siku tano maalumu kwa ajili ya kukamilisha kazi ya 'kuwasuka' wachezaji wake wawe imara kuelekea mechi za mashindano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika.

Yanga inatarajia kuikaribisha Al Hilal katika mchezo wa kwanza wa hatua ya kwanza utakaochezwa Oktoba 8, mwaka huu kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam na marudiano yatakayofanyika Khartoum wiki moja baadaye.

Tayari kikosi cha Al Hilal kimetua mjini Lumbumbashi, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC), ili kuweka kambi ya siku tano na ikipanga kucheza mechi mbili za kirafiki dhidi ya wenyeji, TP Mazembe na AS Vita kabla ya kuifuata Yanga.

Ibenge aliliambia gazeti hili Yanga sio timu ya kuidharau na kuivaa kirahisi kutokana na ubora wa wachezaji walionao na kuhakikisha anajianda vizuri ili kupata matokeo mazuri katika mchezo huo.

Kocha huyo alisema anataka kuona anapata ushindi katika mechi hiyo ya kwanza na baadaye kwenda kumaliza kazi kwenye uwanja wa nyumbani na hatimaye kusonga mbele katika michuano hiyo inayoandaliwa na kusimamiwa kila mwaka na Shirikisho la Soka Afrika (CAF).

Alisema wachezaji wake wanatakiwa kuhakikisha wanacheza kwa utulivu kwa lengo la kupata ushindi na kuifanya mechi ya marudiano kuwa nyepesi.

"Yanga ya sasa sio rahisi, ni timu ambayo inajua kufanya kazi kwa umakini, kuanzia wachezaji mpaka benchi la ufundi, nitakwenda kwa tahadhari kubwa kuhakikisha ninapata matokeo mazuri," alisema Ibenge.

Mkongomani huyo alisema wachezaji wa Yanga anawafahamu wana uzoefu mkubwa na michuano ya kimataifa hivyo watapambana kuhakikisha wanashinda na kuwazidi ataingia uwanjani na mbinu na mipango tofauti ili kufikia malengo yake ya kupata matokeo chanya.

"Kuna baadhi ya wachezaji wa Yanga ninawafahamu kwa sababu nimewahi kuwafundisha, nafahamu ubora na madhaifu yao, kikubwa ni kuendelea kukinoa kikosi changu ili kuhakikisha tunapata matokeo mazuri katika Uwanja wa Benjamin Mkapa," Ibenge alisema.

INAENDELEA UK . 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >